
SIKU YA WANAWAKE

**Kilio** ni kinamama hawajafikia nguvu kamili za kuamua

UKURASA 5



**Mapato** 'kubeti' yapaa, vijana wapewa onyo

UKURASA 3



**Samia** anyoosha kidole sekta ya nishati adha ya kukata umeme

UKURASA 3


# Nipashe

Alhamisi Machi 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 • Na. 0581608

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




TEN HAG HALI TETE UNITED

UKURASA 22



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe

AZIMIO LA MTWARA

# CHADEMA sasa hadi kieleweke

• **Vigogo** wajifungia, Mbowe atoka na hoja 10 mezani za kushinikiza... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 7

## CHANGAMOTO 21 KATI YA 25 ZA MUUNGANO ZATATULIWA



SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimetatua hoja 21 za...

UKURASA WA 22

## PIQUE AITA BARCA KUWAAMBIA UKWELI MASHABIKI

GWIJI wa Barcelona, Gerard Pique, ameionya klabu hiyo dhidi ya kuwahadaa mashabiki wao na kuihimiza klabu...





Viongozi wapya wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mwenyekiti Othman Masoud Othman (kushoto) na Kiongozi wa Chama (KC), Dorothy Semu, wakipunga mikono, baada ya kukamilika kwa Mkutano Mkuu wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Othman, Dorothy wapewa funguo za kuongoza ACT

UKURASA 19

# Vifo tata vya watu wanane, walitetemeka na kuanguka

• **30** hoi wodini, matabibu na polisi waumiza vichwa...*Uk.2*

**MICHEZO** **GAMONDI: LIGI KUU SILAHA TOSHA FAINALI CAF** UK.24 **KABWELA** UK.7

AZIMIO LA MTWARA

# CHADEMA sasa hadi kieleweke

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya kujifungia mjini Mtwara kwa siku kadhaa, vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wametoka na Azimio la Mtwara lenye hoja 10 wanazotaka zifanyiwe kazi kuboresha mfumo wa uchaguzi nchini.

Uongozi wa chama hicho pia umetangaza awamu nyingine ya maandamano yatakayofanyika kwa wiki nzima ifikapo mwezi ujao.

Ni maazimio yaliyotangazwa jana baada ya Kamati Kuu ya chama hicho kujifungia Mtwara, maandamano yakipangwa kufanyika katika kila makao ya makuu ya mikoa yote nchi nzima kuanzia Aprili 22 hadi 30 mwaka huu.

Akisoma maazimio hayo kwa niaba ya Kamati Kuu ya chama hicho jana, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema miongoni mwa mambo wanayoendelea kusisitiza yaboreshwe ni kupatikana Katiba mpya, nchi iwe na tume huru ya uchaguzi na kubadilishwa mfumo mzima wa kusimamia na kuendesha uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Hoja ya pili, Mbowe alisema ni kubadilishwa mfumo mzima wa kutenga majimbo ya uchaguzi ili kuhakikisha yanazingatia idadi sawa ya watu wanaowakilishwa.

"Kuna mbunge wa Dar es Salaam leo anawakilisha wapigakura 500,000 au 600,000, lakini katika nchi hii hii kuna mbunge ambaye anawakilisha watu 30,000. Uwiano uko wapi? Haki iko wapi?

"Tunataka mgawanyo wa majimbo uwe kwa mfumo unaoitwa 'population quarter', ili watanzania wote wawe na haki ya uwakilishi," Mbowe alisema.

Alitaja hoja yao ya tatu ni nchi kuwa na mfumo unaotoa fursa kwa wapigakura wote wenye sifa kwa kuboresha daftari la wapigakura ili kuondoa dosari ambazo hujitokeza wakati wa uchaguzi.

Mbowe pia alisema wanataka kubadilishwa mfumo wa uteuzi wa wagombea ili kuondoa vikwazo vya kuengua wagombea wa upinzani.

Hoja ya tano, Mbowe alisema wameazimia kubadilishwa mfumo wa uendeshaji kampeni za uchaguzi ili kuondoa vitendo vya kunyanyasa wagombea wa vyama vya upinzani na kuwezesha matumizi sawia ya vyombo vya habari.

"Na hapa ninazungumzia zaidi vyombo vya habari vya umma. TBC ni mali ya wananchi wa Watanzania, gazeti Habari la Leo, Daily News, hivi ni vyombo vya habari vya umma, lakini vinatumika kama mali binafsi wakati vinaendeshwa na kodi ya Watanzania wote," alisema Mbowe.

"Sita, tunataka kubadilishwa mfumo mzima wa gharama za uchaguzi na namna ya kuusimamia. Pia tunataka kubadilishwe mfumo mzima unaohusu maadili ya uchaguzi na namna ya kuyasimamia ili kukomesha vitendo vya unyanyasaji wagombea wa upinzani kwa kisingizio cha maadili ya uchaguzi.

"Nane, tumeazimia kuwe na mabadiliko katika utaratibu wa upatikanaji na uapishwaji mawakala wa vyama au wagombea wakati wa kupiga, kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya urais.

"Tisa, tunataka kuwekwa mfumo mpya na bora zaidi wa kutatua migogoro yote ya uchaguzi katika hatua zote za mchakato wa uchaguzi.

"Kumi, tunataka kubadilisha uteuzi wa madiwani wa viti maalum ili kuweka utaratibu wa kikatiba na kisheria utakaowezesha wagombea binafsi kushiriki katika uchaguzi kama wagombea katika ngazi zote za uchaguzi kwenye taifa.

"Tunachokipigania hapa ni uhuru wa watu, matakwa ya kisheria, ulazima wa kugombea kupitia chama cha siasa ni kuwanyima Watanzania uhuru wao.

"Tutatembea mpaka viatu vyote viishe soli, na kama wanafikiri ni masihala waendelee kupuuza, tutaandamana mpaka haki zetu zipatikane na huu ni mwendelezo tu, tunamaliza awamu tunasikiliza mnasemaje, hayo mengine tutatangaziana mbele ya safari, hatua kwa hatua," alisema.

Mbowe alisema chama hicho kiko tayari kwa mazungumzo wakati wote na mazungumzo hayatazuia wala kusitisha maandamano yao.

"Tutaandamana, anayetaka kuzungumza tuzungumze huku tunaaandamana. Mambo ya msingi yakisikilizwa, basi twendeni tukaijenge demokrasia, tukaviandae vyama vyetu kwa uchaguzi, lakini wakiendelea kutupuuza, wakafikiri ni nguvu ya soda, watashangaa," alisema Mbowe.

**DIASPORA**

Mbowe aliema Kamati Kuu ya chama hicho pia imeagiza wanachama wao walioko katika mabara yote duniani, nao wajiandae kufanya maandamano katika miji yote mikubwa duniani.

"Tutaandamana Umoja wa Mataifa, London, Ujerumani, Japan, China, Afrika Kusini, Nairobi, Ufaransa na kila mahali kwa sababu tukikaa kimya tunaoteseka ni mamilioni, wakati wachache wetu wanaendelea kuneemeka katika taifa ambalo ni letu sote.

"Tutazidisha na kuendeleza mapambano hayo hadi hapo madai halali ya muda mrefu ya Watanzania ya kupata Katiba Mpya, mfumo wa kidemokrasia na uchaguzi, Watanzania watakapopata nafuu na hali yao ya maisha na kupunguziwa gharama za maisha, bei za bidhaa na huduma zote muhimu katika maisha yao," alisema.

Mbowe pia alisema wamechoka kuvumilia alichokiita dharau na ukaidi wa serikali kukataa haki na madai yao ya muda mrefu.

Alisema kuwa mwaka 1991, Tume ya Rais ya mfumo wa chama kimoja wa vyama vingi vya siasa, maarufu Tume ya Nyalali, iliyoundwa na Rais Ali Hassan Mwinyi, ilipendekeza kutungwa Katiba Mpya na ya kidemokrasia kwa ajili ya Tanzania.

Alisema tume ililenga mfumo huo mpya wa demokrasia uwe na tume huru, sheria mpya na bora za uchaguzi zitakazohakikisha uchaguzi huru, wa haki na unaoaminika.

Alisema Tume hiyo ilipendekeza kufutwa kwa sheria zote za ukandamizaji na kutungwa sheria mpya zitakazohakikisha kila Mtanzania anapata haki sawa ndani ya taifa lake.

"Serikali si tu imekataa mapendekezo hayo ya Tume ya Nyalali, bali pia imekataa mapendekezo ya mengi yaliyotolewa na tume nyingine nyingi zilizofuata ambazo iliziunda yenyewe," alisema Mbowe.

**MAISHA MAGUMU**

Mbowe pia alisema Kamati Kuu imeelekeza kamati ya wataalamu wa chama hicho kuandaa mpango wa taifa wa kunusuru wananchi dhidi ya ugumu wa maisha, kupunguza bei za vyakula na bidhaa muhimu ambazo alizitaja ni mzigo mkubwa wa maisha magumu unaokabili wananchi.

"Tuliomba serikali itangaze mkatati wa kunusuru wananchi na ugumu wa maisha, lakini haijafanya hivyo.

"Kwa hiyo, licha ya kuwa hatuko serikali, tuna watu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri. Kamati Kuu imeagiza kuandaliwa mpango huo wa kunusuru hali ya ugumu wa maisha unaokabili wananchi kwa sasa," alisema Mbowe.

Tayari chama hicho kimeshafanya maandamano katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha kikishinikiza kufanyika marekebisho ya sheria zinazohusiana na uchaguzi na serikali kuja na suluhisho la ugumu wa maisha unaokabili wananchi kutokana na mfumuko wa bei za bidhaa huku vijana wengi wanaohitimu vyuo vikuu na vyuo vya kati wakikosa ajira.

## TANGAZO LA NOTISI - MDAIWA

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Thelathini (30) kwa mdaiwa Ndugu **BIUSY ANGELA MKUMBWA** wa Kinyerezi Wilaya ya Ilala– Dar Es Salaam .

Biusy Angela Mkumbwa ulikopa na kushindwa kulipa deni la mkopo wako, hivyo unatakiwa kulipa deni lako la mkopo unaodaiwa na Tujijenge ndani ya siku thelathini (30). Hii ni baada ya mkopo kushindwa kulipwa kulingana masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa (siku thelathini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuuza mali zako zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

Kwa Mawasiliano piga:
**+255 222774742-3/0739611612/0718068335**
Au
Email: **tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

## MNADA WA HADHARA

Madalali tajwa hapo chini tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Samwel Ezekiel Masunga | Gari T.977 EEN, TOYOTA HIACE MIN BUS | 22/03/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |
| Afrikana Augustino Mabonya | Kiwanja – Fremu 10, Kivule -Ilala | 21/03/2024 | White Miracle |
| Hans Christopher Mollel | Nyumba – Vijibweni Kigamboni | 26/03/2024 | RAPITECH Solutions Ltd |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.
Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO: 0715683777/ 0716535221**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**White Miracle: 0684937219/0758811276**
**RAPITECH: 0628866132/0755264606**

# Vifo tata vya watu wanane, walitetemeka na kuanguka

**Na Suleiman Rashid Omar,**
PEMBA

HALI ya simanzi imetawala katika Kijiji cha Kisiwa Panza, Wilaya ya Mkoani baada ya watoto 14 kuugua ghafla na watatu kati yao kufariki dunia muda mfupi huku wengine 11 wakilazwa kwa matibabu na uchunguzi katika Hospitali ya Abdalla Mzee.

Hadi jana mchana, idadi ya waliofariki dunia walifikia wanane baada ya wengine watatu kufariki dunia wakiwa hospitalini wakipatiwa matibabu.

Baadhi ya wazazi kisiwani hapo, wakiwa na mfadhaiko, walisema juzi kuwa hawaelewi chanzo cha tatizo hilo ambalo limewakumba watoto wengye umri mdogo ambao asubuhi na mapema walianza kutapika na kutetemeka na baada ya muda mfupi, watatu kati ya hao wakafariki dunia ndipo uamuzi wa kuwapeleka hospitalini ukachukuliwa. Malimu Juma Mati alisema hawajui chanzo cha tatizo hilo na wamepatwa na mshangao kwa kuwa waliokumbwa na ugonjwa huo na wengine kufa ni watoto wenye umri mdogo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Abdalla Hussein Mussa, aliwataja watoto waliofariki dunia kuwa ni Arshad Haji Haji (miaka miwili), Faridat Fumu Khamis (kichanga cha miezi mitatu) na Kazima Makame Haji (miaka minne) wote wakazi wa Kisiwa Panza.

Aliwataja waliolazwa kuwa ni Aviwe Khamis Khalfan (miaka miwili), Abubakar Makame (mwaka mmoja na nusu) Azikar Haji Haji (6), Suleiman Haji Hamad (12), Samira Haji Hamad (12), Fatma Suleiman Hamad (11) na Sahira Khamis Makame miaka miwili.

Wengine ni Biabu Abdalla Juma (37), Mati Vuai Mohamed (8), Fakih Vuai Mohamed (6) na Hulaiafa Ame Othman (18) wote wakazi wa Kisiwa Panza ambao wote wanaendelea na matibabu.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Khamis aliwataka wakazi wa Kisiwa Panza na maeneo jirani kuwa watulivu wakati huu ambao uchunguzi unafanyika ili kujua chanzo cha tukio hilo.

Kaimu Daktari Mfawidhi wa Hospitali ya Abdallah Mzee, Mohamed Faki Salehe, alisema walipokea wagonjwa 33, watano wamefariki dunia na wengine walifariki kijijini na kufanya jumla ya wanane.

"Idara ya Kinga Wilaya ya Mkoani imefunga kambi katika eneo la Kisiwa Panza ili kutoa matibabu pale pale, wamesema uchunguzi wa awali wamegundua vimelea vya bakteria vinavyosababisha matatizo, ila uchunguzi zaidi wanafanya kwenye maabara kubwa," alisema.

# Mapato ya 'kubeti' yazidi kupaa, vijana waonywa

**Na Restuta James**

MAPATO yatokanayo na michezo ya kubahatisha yamepanda kutoka Sh. bilioni 2.8 mwaka 2006/07 hadi Sh. bilioni 170.4 mwaka 2022/23.

Kukishuhudiwa ongezeko hilo la mapato, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) imetahadharisha vijana na wapenzi wa michezo hiyo kwamba si kazi wala chanzo cha mapato, bali ni burudani.

Michezo hiyo pia imezalisha ajira 25,000, huku Tanzania ikitajwa kuwa mfano wa kuigwa kwa usimamizi mzuri wa burudani hiyo kwa nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari, akisisitiza michezo ya kubahatisha ikiwamo ya kubashiri matokeo ya mpira wa miguu ni burudani.

"Ningependa umma ufahamu kuwa watoto na vijana chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kushiriki. Ushindi katika michezo ya kubahatisha ni kwa bahati na si mbinu yoyote na ndio maana tunasema hii si ajira wala haipaswi kuchukuliwa kama chanzo cha mapato, hii ni burudani," alisema.

Mbalwe alisema pamoja na kwamba ni burudani, mpenzi wa michezo hiyo anapaswa kucheza kwa kiasi ili asipate uraibu.

"Hadi Juni 2023, GBT imesajili kampuni 91 zinazoendesha aina mbalimbali za michezo ya kubahatisha. Tunapenda kusisitiza kuwa michezo hii haipaswi kuendeshwa karibu na nyumba za ibada, maeneo ya shule na usalama, yasiyofikika kirahisi na ni lazima yasajiliwe na bodi," alisema Mbalwe.

Kuhusu mchango wa michezo ya kubahatisha, alisema kumekuwa na ongezeko la kodi, akitolea mfano mwaka kodi ya Sh. bilioni 33.6 mwaka 2016/17 na Sh. bilioni 170.4 kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 407.1 katika kipindi hicho.

Alisema katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Disemba mwaka jana, kodi iliyokusanywa ni Sh. bilioni 108 na matarajio ni kupata Sh. bilioni 200 katika mwaka huu wa fedha.

Alisema mchango mwingine ni asilimia tano ya mapato yatokanayo na kubashiri matokeo kwenye mpira wa miguu kupelekwa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) kwa ajili ya kukuza sekta ya michezo nchini.

Mkurugenzi huyo alisema sekta ya michezo ya kubahatisha inakabiliwa na kuwapo mashine za kamari zinazoingizwa nchini na watu wasiosajiliwa, jambo linaloikosesha nchi mapato.

Mbalwe alisema kuwa kati ya mwaka 2018/19 na Agosti 2022, GBT ilikamata mashine 1,846 za kamari katika maeneo mbalimbali nchini, ambazo kama zisingedhibitiwa, zingeikosesha nchi mapato ya Sh. bilioni 2.44 kwa mwaka.

Alisema GBT inakusudia kuendelea kusimamia kwa karibu sekta hiyo ili isiathiri jamii hasa vijana na watoto, kuiendesha kwa uwazi na uaminifu ili washindi wapate haki yao na kuelimisha wananchi kuhusu michezo ya kubahatisha.

Kwa mujibu wa Mbalwe, mikoa inayoongoza kwa wakazi wake kushiriki michezo ya kubahatisha ni Dar es Salaam, ukiongoza pia kwa miamala na makusanyo ya kodi, ukifuatwa na mikoa ya Arusha na Mwanza.

Baadhi ya wahariri na waandishi walishauri bodi hiyo kusimamia sheria kikamilifu na kufanya utafiti ili kuongeza udhibiti wa michezo hiyo.

GBT imetaja aina ya michezo ya kubahatisha ni kasino kwenye majumba maalum na mtandaoni, mashine za kamari, ubashiri wa matokeo ya michezo, ujumbe mfupi wa simu, maduka ya mashine arubaini na bahati nasibu ya taifa.

# Samia anyooshea kidole sekta ya nishati adha kukata umeme

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Nishati kuongeza umakini katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta ya nishati na kuwahudumia Watanzania ipasavyo ili kuondoa manung'uniko kutokana na kukatika kwa umeme bila taarifa maalum.

Agizo hilo alilitoa juzi Ikulu Ndogo ya Tunguu, Zanzibar, wakati wa hafla ya uapisho wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya hiyo, Dk. James Mataragio, aliyeteuliwa hivi karibuni akichukua nafasi ya Athuman Mbuttuka ambaye uteuzi wake ulitenguliwa.

Rais alisema kutokana na sekta ya nishati kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya kiuchumi na maisha ya kila siku ya mwanadamu, ni muhimu kuwekewa umakini katika usimamizi wake kwa kuhakikisha watendaji wanatekeleza wajibu wao ipasavyo.

Pia alisema wizara hiyo, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) zinapaswa kuwa na mwendelezo wa utoaji wa taarifa ndani ya serikali na kwa umma juu ya kuwapo kwa hitilafu na matengenezo ili kuondoa sintofahamu kwa Watanzania.

Alisema sekta hiyo inahitajika watumishi kutimiza wajibu wao kwa uzalendo mkubwa na kwa kuzingatia kanuni zote za utunzaji wa mitambo na miundombinu inayotoa Nishati ili iwe kwenye hali nzuri wakati wote.

Vilevile aliitaka wizara kutengeneza mpango maalum wa usambazaji wa gesi ili iwe rahisi kualika sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kufikia lengo lililokusudiwa la asilimia 85 ya kaya zote kutumia Nishati safi ifikapo mwaka 2031.



Alisema kuna nchi zilizoonesha nia ya kufanya kazi na Tanzania katika masuala ya gesi hivyo ni muhimu kuangalia sharia na miongozo inayoifunga serikali kukaribisha sekta binafsi na kuifanyia marekebisho.

**MAFUTA BEI JUU**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza bei mpya elekezi za mafuta ya petroli, dizeli na taa, kuanzia Machi 6, mwaka huu, huku bei ya rejareja, petroli na dizeli zikipanda.

Bei ya rejareja ya petroli kwa mkoa wa Dar es Salaam, imepanda kutoka Sh. 3,051 hadi Sh 3,163 kwa lita moja sawa na ongezeko la Sh. 112 kwa lita.

Kadhalika bei ya dizeli, imepanda kutoka Sh 3,029 hadi Sh 3,126, sawa ongezeko la Sh. 97 kwa lita huku mkoani Tanga, petroli ikipanda kutoka Sh. 3,064 hadi Sh 3,209.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Mwainyekule, aliyasema hayo katika taarifa yake jana, kwa umma kuhusu bei kikomo za bidhaa hiyo nchini, kuanzia Jumatano, Machi 6, mwaka huu.

"Mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi Machi 2024 yamechangiwa na ongezeko la bei za mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia (FOB) kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mafuta ya petroli na asilimia 1.99 kwa mafuta ya dizeli na kupanda kwa gharama za uagizaji wa mafuta kwa Bandari ya Dar es Salaam.

"Imepanda kwa wastani wa 15.38 kwa petroli na asilimia 40.41 kwa dizeli na kwa Bandari ya Mtwara kwa wastani wa asilimia 7.61 kwa petroli na dizeli. Mabadiliko ya bei za mafuta yamechangiwa pia na ongezeko la matumizi ya EURO katika kulipia mafuta yaliyoagizwa," alisema.

Alisema kwamba wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zilizoainishwa na EWURA na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka agizo hilo.

"EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja kwa mamoja na jamii. Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko.

"EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa bei hizo zisizidi bei kikomo (Price cap) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa," aliongeza.

**•Imeandikwa na Vitus Audax na Christina Mwakangale**


## Uteuzi wa Bw. Justice Novati Rutenge kama Mkurugenzi Mtendaji Mpya wa FCS

fcs
FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY



JUSTICE RUTENGE
Executive Director, FCS

STAY CONNECTED
@FCSTZ

Bodi ya Wakurugenzi ya Foundation for Civil Society (FCS) inayofuraha kumtangaza Bw. Justice Novati Rutenge kama Mkurugenzi Mtendaji mpya wa FCS, kufuatia mchakato wa takribani miezi mitano wa kutafuta kiongozi mpya.

Bw. Rutenge ni mtaalamu na mbobezi wa maswala ya maendeleo mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 13 katika maswala ya utawala bora, maendeleo ya sekta binafsi, kilimo, afya na elimu. Katika kipindi cha miaka 10, Bw. Rutenge amekua Mshauri Mwelekezi Mkuu katika taasisi za iDev Tanzania Ltd na iDev Consulting. Alianzisha makampuni hayo akiwa na shauku ya kutumikia sekta ya maendeleo ya kimataifa kupitia ujuzi wake wa ubunifu na uchambuzi. Katika kipindi hiki, ameshauri mashirika mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Asasi za Kiraia za kitaifa na kimataifa, wafadhili, mashirika ya kimataifa, mashirika ya uhisani wa kimataifa, na makampuni binafsi. Bw. Justice amefanya kazi na FCS kwa takribani miaka 7 kama mshauri mwelekezi na ameisaidia FCS katika maswala ya upimaji wa matokeo; uundaji wa programu na mipango mikakati mbalimbali; mawasiliano ya kimkakati; na katika kutafuta rasilimali fedha za shirika.

Bw. Rutenge ana Shahada ya Kwanza ya (BA) katika Maendeleo ya Jamii kutoka Chuo Kikuu cha Daystar, Shahada ya pili (MSc) katika Mawasiliano na Maendeleo kutoka Chuo cha London School of Economics and Political Science (LSE) na kwa sasa anaendelea na masomo ya shahada ya uzamivu (PhD) katika Biashara na Menejimenti katika Chuo Kikuu cha Strathmore.

Tangu 2016, ameandika makala zaidi ya 50 zilizoangazia masuala mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika vyombo vya habari kadhaa. Kazi yake imemwezesha kuchaguliwa kuwa mshiriki wa programu kama Mandela Washington Fellowship katika Mpango wa Viongozi Vijana wa Afrika (YALI), pamoja na Programu ya Kuendeleza Uongozi wa Afrika (PfAL) katika Chuo cha London School of Economics and Political Science (LSE).

Bw. Rutenge anachukua nafasi ya uongozi katika FCS katika wakati muhimu wa mabadiliko ya mienendo ya sekta na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoenda kwa kasi. Anaungwa mkono kikamilifu na Wanachama na Bodi ya FCS kuongoza katika nyakati hii, na kuimarisha nafasi ya FCS kama mwezeshaji wa maendeleo yanayozingatia watu nchini Tanzania, pamoja na kua sauti muhimu katika mijadala ya maendeleo ya kimataifa.

Pia natumia fursa hii kumshukuru sana Bw. Francis Kilian Kiwanga ambaye anamaliza muda wake tarehe 30 April 2024. Katika uongozi wake ametoa mchango mkubwa katika uongozi wa shirika letu kwa Miaka 9. Katika kipindi chake cha uongozi shirika limepiga hatua kubwa ya maendeleo na kufikia malengo kulingana na mipango yetu. Pia, tumejenga misingi mizuri ya mahusiano na serikali, wadau wa sekta binafsi na wadau wa maendeleo.

Tunawaalika wadau wetu wote na umma kwa ujumla kumpa Bw. Rutenge na menejimenti mpya ya FCS ushirikiano unaohitajika wanapotekeleza majukumu yao.

Bw. Rutenge ataanza jukumu lake jipya tarehe 1 Mei, 2024, akimrithi Bw. Francis Kiwanga na anakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa wanne tangu FCS ianzishwe mwaka wa 2002.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131(1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni | Aina ya Ombi la Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ultimate Oil and Gas Tanzania Limited, S.L.P 8938, Dar es Salaam. | Eneo la Mikocheni "A", Kinondoni, Dar es Salaam. | Emmanuel Kawedi Shayo (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 2. | Xenom Energy Limited, S.L.P 42935, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. G6, Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Kevin Ochieng Owino (Raia wa Kenya) | Leseni ya jumla ya Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 3. | Gas Care (T) Limited, S.L.P 3476, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 10, Eneo la Kisutu, Ilala, Dar es Salaam. | Mohamed Abdullahi Sirad (Raia wa Kenya) | Leseni ya jumla ya Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 4. | Tazama Pipelines Limited, S.L.P 2157, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1/1/2, Eneo la Tungi, Kigamboni, Dar es Salaam. | Patrick Musenyesa (Raia wa Zambia) | Leseni ya jumla ya Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 5. | Admire Lubricant and Services Limited S.L.P. 7494, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 38, 39, 40 & 41, Eneo la Gerezani, Ilala, Dar es Salaam. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi | Ombi la Leseni Mpya |
| 6. | Hesu investment limited, S.L.P 2464, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 311/4, Eneo la Chang'ombe, Temeke, Dar es | Maduhu Gilya Manyangu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa matumizi binafsi (Transporter) | Ombi la Leseni Mpya |
| 7. | Shaddle Flour Mills, S.L.P 19600, Dar es Salaam. | Eneo la Kariakoo, Ilala, Dar es Salaam. | Shedrack January Mutembeyi (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya kupikia | Ombi la Leseni Mpya |
| 8. | Africa Energy Ltd. S.L.P 522786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 44 45, Eneo la Sokota, Temeke, Dar es | Edhah Abdallah Munif (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 9. | Lake Oil Limited Tabata Darajani, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 270 & 272, Eneo la Tabata Mawenzi, Ilala, Dar es | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 10. | Lake Oil Limited Yombo Buza, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2689, Eneo la Yombo Buza, Ilala, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 11. | Puma Kawe Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 703, Eneo la Kawe, Kinondoni, Dar es Salaam. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 12. | Victoria Service Station-Mabibo Mandela Road Service Station, S.L.P 75467, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 9/3, Kitalu "C", Eneo la Ubungo – Makuburi, Ubungo, Dar es Salaam. | Harold Elisamehe Matemba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 13. | Victoria Service Station – Mabibo Mandela Road Service Station, S.L.P 75467, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 9/3, Kitalu "C", Eneo la Ubungo – Makuburi, Ubungo, Dar es Salaam. | Harold Elisamehe Matemba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 14. | Herbert Enock Daffa – K. B Service Station, S.L.P 64, Korogwe. | Kiwanja Na. 225, Eneo la Goba Kisauke, Kinondoni, Dar es | Herbert Enock Daffa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la kuhuisha Leseni |
| 15. | Puma Energy Tanzania Limited-Bagamoyo, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Eneo la Zinga, Bagamoyo, Pwani. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 16. | Lake Oil Limited Mkuranga, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Eneo la Mkuranga, Mkuranga, Pwani. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 17. | Aisha Iddi Mtaula – Miono Filling Station S.L.P 48 Chalinze | Kiwanja Na. 1, Kitalu "B", Eneo la Miono, Chalinze, Pwani. | Aisha Iddi Mtaula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 18. | Kisemvule Petroleum Products Ltd, S.L.P 1117, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 10, Eneo la Kisemvule, Mkuranga, Pwani. | Said Salim Bathawab (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 19. | Pyramid Oil Company Limited, S.L.P 2473, Dodoma. | Kijiji cha Kibondeni, Kibaha, Pwani. | Sebastian John Luena (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 20. | Mansoor Industries Ltd – Visiga, S.L.P 80218, Dar es Salaam. | Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Shanif M Jamal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 21. | Acer Petroleum (T) Ltd – Tandahimba, S.L.P 78845, Mtwara. | Kiwanja Na. 703, Kitalu "C", Eneo la Mji mwema, Tandahimba, Mtwara. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 22. | KSM Filling Station, S.L.P 108. Tunduru. | Kiwanja Na. 59, Kitalu "A", Eneo la Masista, Namtumbo, Ruvuma. | Said Shaibu Kazibure (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 23. | GMS Oil & Lubricants Co. Ltd – Mbinga Petrol Station, S.L.P 681,Songea. | Kiwanja Na. 18, kitalu "B", Eneo la Lusaka "B", Mbinga, Ruvuma | George Abraham Mwalongo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 24. | KBG Logistics Co. Limited, S.L.P 4604, Mbeya. | Kijiji cha Itamboleo, Mbarali, Mbeya | Keneth Beny Goliama (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 25. | Rutala Limited, S.L.P 668, Mpanda. | Eneo la Laela, Sumbawanga, Katavi. | Lazaro Jacob Twange (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 26. | Mansoor Industries Limited, S.L.P 2860, Mwanza. | Kiwanja Na. 1449, Kitalu "M", Eneo la Sabasaba, Ilemela,Mwanza. | Shanif Mansoorali Jamal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 27. | Shija Saimon Kadiko, S.L.P 44, Buchosa. | Kijiji cha Mwabasabi, Nyehunge, Buchosa, Mwanza. | Shija Saimon Kadiko (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 28. | Engen Petroleum (T) Limited, S. L. P. 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 7 Kitalu "BB" Eneo la Mabatini, Nyamagana, | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 29. | Zanzibar Charles Kabale, S.L.P 51, Bukombe. | Eneo la Buganzu – Uyovu, Bukombe, Geita. | Zanzibar Charles Kabale (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 30. | Quick Services Station Co. Limited, S.L.P 34, Muleba. | Kijiji cha Kakubilo, Geita. | Beach Evarist Makaga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 31. | Olympic Petroleum(T) Limited, S.L.P 6185,Mwanza. | Kijiji cha Bukima, Musoma, Mara. | Ally Mohamud Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 32. | Mariki Enterprises Limited S.L.P 8915 Moshi | Shamba Na. 1225, Eneo la Maji ya Chai, Arumeru,Arusha. | Tadei Ansel Mariki (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 33. | Hydom Traders Limited, S.L.P 9000, Hydom. | Kijiji cha Bassotu, Hanang, Manyara. | Yuda Edward Munyaw (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 34. | New Salama Esso Service Station – Tanga Branch, S.L.P 5713,Tanga. | Kiwanja Na. 8, Kitalu "130540", Barabara ya Pangani, Tanga. | Gulammehdi Mohamedjaffer Pira (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la kuhuisha leseni |
| 35. | Mlowa Filling Station, S.L.P. 342, Dodoma | Kiwanja Na. 4, kitalu "BD", Eneo laMakulu, Dodoma. | Cosato chumi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 36. | Florian Msuluza-Diza Filling station, S.L.P. 77, Mlimba. | Kiwanja Na. KB/CHT/SQ188, Eneo la Mlumbaji, Kilombero, Morogoro. | Florian Daudi Msuluza (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma. Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030; Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

# Mifumo, kikwazo wanawake kufikia nafasi za uamuzi

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, wadau wa maendeleo ya wanawake wametaka kuwekwa mifumo rasmi na wezeshi ya kikatiba, kisheria na kisera ya usawa katika nafasi za uongozi ili kuondoa mila kandamizi, desturi na mitazamo hasi dhidi ya ushiriki wa wanawake katika maamuzi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku hiyo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, alisema bado kuna mila kandamizi na mitazamo hasi katika jamii kuhusu ushiriki wa wanawake kugombea nafasi za uongozi ambayo inapaswa kuondolewa kwa kutungiwa sheria, kuwekewa sera au kuwekewa mifumo wezeshi katika Katiba.

"Ukatili wa jinsia hususan ule wa kingono pamoja na rushwa ya ngono ni kikwazo kwa wanawake kushika nafasi za uongozi, uwezo mdogo wa kiuchumi pia unawakwamisha wanawake kushiriki kutafuta nafasi za uongozi hususan katika siasa," alisema Mkurugenzi Liundi.

Alitaka pawepo utashi wa kisiasa na dhamira ya kweli kwa viongozi wa vyama vya siasa kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi ndani na nje ya vyama hasa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, mwaka huu na uchaguzi mkuu, mwakani.

Wadau hao pia waliibua tatizo la umiliki wa rasilimali mbalimbali hasa ardhi ya kuwa bado ni shida kwa wanawake kutokana na mila na tamaduni za jamii zinazompa nafasi zaidi mwanamume katika kumiliki ardhi jambo ambalo alisema linarudisha nyuma maendeleo ya mwanamke kiuchumi.

"Umiliki wa ardhi kwa wanaume ni asilimia 75 ukilinganisha na asilimia 27 kwa wanawake. Wanawake wenye umiliki wa ardhi wengi wao wanatumia kwa kulima mashamba madogo madogo kwa kuzalisha mazao ya chakula kwa ajili ya familia," alisema.

Tatizo la upatikanaji wa huduma bora za kijamii alitaja kuwa bado ni kikwazo kingine katika kukuza maendeleo ya wanawake akitolea mfano ukosefu wa huduma ya majisafi na salama inawaongezea wanawake na wasichana mlundikano wa majukumu na kushindwa kushiriki katika shughuli nyingine za kukuza uchumi za siasa husuan uongozi wa kisiasa.

Katika hatua nyingine, kasi ya wanawake kuanzisha biashara kubwa na kuzisimamia imeifurahisha serikali na kutaka uwekezaji zaidi kwa kundi hilo ili kukuza maendeleo, ustawi wa jamii na kujenga familia bora kwa maslahi mapana ya taifa.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana katika mkutano wa sita wa Mwanamke Kiongozi Mwaka 2024 na mahafali ya tisa ya Programu ya Mwanamke Kiongozi, ulioandaliwa na Chama cha Waajiri (ATE).

Dk. Gwajima alisema uwekezaji kwa mwanamke ni kuunga mkono juhudi kubwa za serikali iliyochukua hatua kadhaa za kuboresha kipato na kuondoa umaskini kwa kundi hilo kwa kutoa fursa za kiuchumi na elimu kwa watoto wa kike.

Alitoa rai kwa ATE kuendelea kutoa mafunzo hayo ya uongozi kwa wanawake pamoja na kuendelea kuwa vinara katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa maeneo ya kazi.

Dk. Gwajima aliwaasa wanawake kushikamana na kwa walioko maeneo ya kazi, wahakikishe wanawanyanyua wengine kwa kuwasaidia badala ya kuwa, visababishi vya misongo ya mawazo.

Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran, alitoa rai kwa waajiri kuendelea kuweka mikakati na jitihada kufikia usawa wa kijinsia hususani kwa nafasi za bodi za wakurugenzi na za juu za uongozi.

Aliwataka wahitimu wa programu hiyo kuweka juhudi na tija na kuishi katika mafunzo waliyopatiwa na kutumia nafasi zao za uongozi kuleta mafanikio katika sehemu zao za kazi na kwa jamii inayowazunguka.

"Mikutano hii tumekuwa tukiiratibu na kufanyika sanjari na mahafali katika wiki ya Siku ya Mwanamke Duniani. Kaulimbiu ya mkutano huu inasema, "Wekeza kwa Wanawake: Ongeza Kasi ya Maendeleo," alisema.

Suzanne alisema juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia, zinajidhihirisha kwa kuendelea kuweka wanawake katika nafasi mbalimbali za uamuzi.

Wakati huo huo, Shirika lisilo la kiserikali la Legal Services Facility (LSF) na Enabel, Shirika la Maendeleo la Ubelgiji wametia saini mkataba wa ruzuku ya Sh. bilioni 10.7 kwa lengo la kuimarisha huduma ya upatikanaji wa haki kwa wanawake kupitia msaada wa kisheria.

Mradi huo shirikishi unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya mradi wa "Gender Transformative Action: Breaking the Glass Ceiling" wenye lengo la kupunguza unyanyasaji wa kijinsia na kuongeza usawa katika upatikanaji wa haki hususani kwa wanawake na wasichana.

Katika hafla ya utiaji saini mkataba huo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema kupitia mradi huo, LSF itahakikisha kuwa huduma za msaada wa kisheria zenye ubora zinapatikana kwa watu wote kupitia mifumo rasmi na isiyo rasmi ya utoaji haki.

Lulu alisema mradi huo utaongeza uelewa wa jamii hususani wanawake na wasichana kuhusiana na umuhimu wa msaada wa kisheria.

Mwakilishi Mkazi wa Enabel nchini Tanzania, Koenrad Goekint, alisema ushirikiano huo muhimu na LSF ni wenye nia ya kuimarisha upatikanaji wa haki, hasa kwa wanawake, wasichana na jamii zilizotengwa.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Enock Charles**

# 'Wanaojifungua watoto njiti waongezewe likizo'

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), kimeiomba serikali kufanya mabadiliko katika sheria zake ili kuwaongezea muda wa siku za likizo ya uzazi wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.

Lengo ni kutoa fursa ya kuwahudumia watoto hao na kupata muda wa kupumzika ili wanaporejea kazini waweze kulete tija katika maeneo yao ya kazi.

Ofisa Elimu Kazi wa TUGHE, Nsubisi Mwasandende, aliyasema hayo juzi walipotembelea na kutoa msaada katika wodi ya wanawake waliojifungua watoto njiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi.

Mwasandende akiwa na ujumbe wa wawakilishi kutoka Kamati ya Wanawake TUGHE, Makao Makuu pamoja na uongozi wa chama hicho Mkoa wa Pwani, alisema sheria ya sasa ya ajira na uhusiano kazini imekuwa ikitoa siku 84 kwa wanawake wanaojifungua mtoto mmoja.

Pia, alisema hutoa siku 100 kwa wanaojifungua zaidi ya mtoto mmoja na wala haisemi chochote kuhusiana na wanawake wanaojifungua watoto njiti, hivyo TUGHE imeona ni vyema kuendelea kuikumbusha serikali kufanya mabadiliko kwa kuongeza kipengele kuhusu kuongezewa siku za likizo ya uzazi kwa wanawake wanaojifungua watoto njiti.

"Wapo wanawake wengi watumishi wamekuwa wakijifungua watoto njiti na muda wanaopata kukaa na watoto unakuwa hautoshi, kwa kuzingatia watoto hao huitaji sana uangalizi wa karibu kutoka kwa mama zao ili waweze kukua na pia, afya zao kuimarika.

"Tunaomba serikali iliangalie upya jambo hili kwa kufanya mabadiliko katika sheria zake," alisisitiza Mwasendende.

Kuhusu sekta binafsi, Mwasandende aliwaomba waajiri katika mikataba yao ya hali bora kuingiza kipingele hicho cha kuongeza muda kwa siku za likizo ya uzazi wanaojifungua watoto njiti kama mwishoni mwa mwaka jana TUGHE kiliweka kipengele hicho katika mkataba wake wa Hali Bora.

Mwenyekiti wa Wanawake TUGHE, Makao Makuu, Agness Ngereza, alisema katika kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, wameona ni vyema kuwatembelea na kutoa msaada kwa wanawake hospitalini hapo waliojifungua watoto njiti.






Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa hatua aliyochukua Rais Samia viongozi hawana budi kujitafakari

**KATIKA** kuhakikisha kero za wananchi zinapatiwa ufumbuzi, Rais Samia Suluhu Hassan, ametangaza kutenga siku moja kila mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero za mwananchi mmoja mmoja, ambao atakutana nao katika ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) zilizoko Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. Ratiba ya kukutana na wananchi hao itategemea mahali atakakokuwako kwa wakati husika.

Hatua hiyo ya Rais kukutana na wananchi, ilitangazwa juzi na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM anayeshughulikia Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam. Makonda katika taarifa yake alisema Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, ameamua kufanya hivyo ikiwa sehemu ya kuwaonyesha viongozi wa chini yake namna bora ya uwajibikaji.

Kwa mujibu wa Makonda, viongozi wa ngazi za juu CCM walikwenda mikoani na katika ziara zao, walibaini mambo mengi yanayowahusu wananchi ambayo hayajafanyiwa kazi, hivyo kuonyesha kwamba hakuna uwajibikaji katika ngazi za mikoa na wilaya hususani usikilizaji wa kero za wananchi. Kwa mantiki hiyo, Rais Samia ameamua kuonyesha kwa vitendo namna ya uwajibikaji hasa utatuzi wa kero za wananchi kwa kukutana nao na kuwasikiliza kisha kumpa kazi ya utekelezaji mtu anayesimamia sekta husika.

Kwenye ziara za Makonda alizozifaya katika mikoa kadhaa hivi karibuni, mambo mbalimbali yaliibuliwa kutoka kwa wananchi hali iliyoonyesha kwamba kuna uonevu, unyanyasaji, dhuluma na matumizi ya nguvu dhidi ya wananchi. Kutokana na hoja zilizoibuliwa na wananchi kwenye ziara hizo, ilionekana wazi kwamba baadhi ya viongozi wanashirikiana na vyombo vya dola hususani polisi katika kupoka haki za wananchi.

Migogoro mingi iliyoibuliwa na wananchi inahusu ardhi, watu kusingiziwa kesi kuhusu mambo mbalimbali na mengi yalionekana kufanywa na watu wenye nguvu ya fedha katika kuwapoka haki wananchi. Moja ya mifano hiyo ni katika sekta ya ardhi ambapo baadhi ya maofisa katika halmashauri walidaiwa kushirikiana na watu wenye fedha katika kutwaa maeneo ya wananchi au kuwamilikisha ardhi watu zaidi ya mmoja katika eneo moja.

Hayo yote yalibainika baada ya ziara zilizofanywa katika mikoa 23 kwenye mikutano 247 ya hadhara, zilitolewa zaidi ya kero 2,000 nyingi zikielekezwa katika sekta ya ardhi ambako mabavu zaidi yalitumika kwa wananchi kuporwa maeneo yao na kumilikishwa watu wenye uwezo wa kifedha.


Viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia sekta husika zilizolalamikiwa walipopewa nafasi ya kujibu masuala yaliyoibuliwa, walionekana kushindwa kutoa majibu ya msingi hali iliyoonekana kuwa wanahusika katika matatizo yaliyopo. Kwa mantiki hiyo, Rais Samia ameona kuna tatizo kwa wateule wake wengi kwenye ngazi za mikoa na wilaya, hivyo kuamua kuonyesha mfano wa uwajibikaji kwa kusikiliza kero za wananchi kulingana na ratiba atakayopanga.

Kwa hatua aliyochukua Rais, ni wazi kwamba kuna ombwe la uongozi katika baadhi ya maeneo ya kimamlaka na hiyo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na watu kutojua wajibu wao katika mujukumu yao ya kila siku. Watu wanapewa kazi lakini wanashindwa kutimiza dhana kuu kwamba uongozi ni dhamana na wako kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero zinazowahusu wananchi.

Hiyo pia inajionyesha wazi wakati wa ziara za viongozi kwenye mikoa na wilaya wanapopokewa kwa mabango yanayoeleza kero mbalimbali wanazozipata. Kubwa zaidi hiyo inaonyesha kwamba wako viongozi waliopewa dhamana na kuwaongoza wananchi ikiwamo kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Kutokana na ukweli huo, viongozi katika ngazi za mikoa na wilaya, hawana budi kujitafakari upya juu ya wajibu wao na kama viatu walivyopewa vinawatosha. Kama haviwatoshi ni vyema wakaachia ngazi badala ya kutumbuliwa na kupata fedheha katika jamii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Hili la 'elimu bila ukomo', kongole kwenu maprofesa waongoza wizara

**WIKI** iliyopita, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, aliwaomba wadau wa maendeleo kuendelea kushirikiana na serikali pamoja na taasisi zake, ili kuleta mabadiliko endelevu katika sekta ya elimu kwa ujumla.

Hapo, alimwakilisha Waziri wa Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda. Jambo lililonivuta zaidi, ni kwamaba siku hiyo alizundua Kongamano la Elimu Bila Ukomo mwaka 2024.

Prof. Carolyne anasema, serikali ya imeweka dhamira ya dhati ya kuendeleza elimu nchini, hapo anasisitiza hilo limedhihirika kutokana na kukamilika maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, pamoja na mitaala ijayo.

"Sisi kama wizara tunaona fahari kubwa kwa kazi kubwa iliyofanyika na tuna imani kuwa utekelezaji wa mabadiliko yaliyofanyika utaleta mapinduzi ya kielimu na kijamii nchini.

"Mabadiliko ya mitaala hayapaswi kuishia kwenye mfumo rasmi pekee yanatakiwa, pia katika sekta ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi vilevile" anasema

Anaongeza kuwa, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023, pamoja na malengo mengine, imelenga kukuza fursa za elimu isiyo na ukomo kwa watu wote, na kujenga Watanzania mwenye utamaduni wa kupenda kujisomea na kujiendeleza katika muktadha huo.

Anakumbusha kuwa, sera hiyo pia inatoa msimamo kwamba. elimu nje ya mfumo rasmi itatambuliwa na watakaopitia mfumo huo, watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu, kulingana na vigezo vitakavyowekwa.

Katibu Mkuu anafafanua kwamba, sera imeweka uthitishio kuwa, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kuimarisha na kusimamia afua mbalimbali zinazolenga kutoa fursa za elimu kwa wale walioikosa.

"Katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023, dhana inayotawala ni ile ya elimu bila ukomo. Kwa hiyo, elimu ya watu wazima inapewa nafasi kubwa zaidi, inaandaa jamii kupata stadi za msingi za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, na stadi za maisha.

"Inatoa fursa ya kuwa na jamii inayojali na kuthamini elimu, kwa kuhakikisha watoto wanaandikishwa na kuwawezesha kufanya vizuri katika masomo. Pia, inatoa fursa kwa walioikosa ili kupata elimu kupitia elimu nje ya mfumo rasmi" anasema Prof. Calolyne, katika kongamano hilo lililowakutanisha wadau wa elimu jijini Dar es Salaam

Hata hivyo, aliwasihi waliohudhuria katika kongamano hilo kufanya mjadala mpana wa kitaifa ili kupata mawazo ya namna bora ya kutekeleza shughuli za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, sambamba na mabadiliko ya sera mpya ya elimu.

Prof. Carolyne, anasema kwa sasa, serikali inataka elimu ya watu wazima ilenge mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mtazamo wa sasa, kama ulivyosisitizwa katika sera mpya ya elimu.

"Ndugu Mwenyekiti wa Kongamano, kwa kuzingatia kaulimbiu ya kongamano hili, mabadiliko ya sera ya elimu nchini, fursa na changamoto katika utoaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi, nimefurahi kuwa mjadala wetu utachokozwa na wawasilisha mada waliobobea katika maeneo yao ya taaluma na utaalamu.

"Nimefurahi mada zimeandaliwa kuvutia mjadala katika maeneo ya kisheria, muundo wa kitaasisi, uzoefu kutoka nchi zingine na ushiriki wa sekta binafsi na asasi za kiraia.

"Maeneo haya ni muhimu, ili kuwa na elimu ya watu wazima yenye mchango mkubwa zaidi kwa maendeleo ya taifa" anasema

Ni jambo linaloungwa mkono na Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Prof. Michael Ng'ubi, akinena kwamba elimu bila ya ukomo, itamuwezesha Mtanzania kusoma tangu anapozaliwa mpaka mwisho wa maisha yake.

"Wajibu wa wananchi ni kubadilisha mtazamo, hakuna tofauti kati ya kusoma na kuishi. Ilizoweleka kwamb,a mtu akifikia kiwango fulani cha elimu, anaacha kusoma anaanza kutafuta maisha.

"Ndio maana hapa Wizara ya Elimu, kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima tunakwenda kutengeneza miongozo na utaratibu utakaompa mwanafunzi fursa ya kuendelea kijifunza muda wote," anasema Prof Ng'umbi.

HABARI KITAIFA

# Adaiwa kupoka maeneo ya wafugaji, DC adai hajaarifiwa

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAKAZI wa Kitongoji cha Misani, Kata ya Kiwangwa, wilayani Bagamoyo wameomba serikali kuingilia kati kwa kudhibiti uvamizi wa ardhi unaofanywa katika eneo lao la makazi na mifugo.

Wamedai kuna mtu amekuwa akijitwalia ardhi kwa nguvu huku akiwatishia kwa silaha za moto anapotekeleza adhma yake ya kukata miti na kujenga vibanda vyake kama ishara ya kumiliki eneo husika.

Wananchi hao ambao ni jamii ya wafugaji walieleza waandishi wa habari kijijini huko juzi kuwa eneo hilo licha ya kutengwa kwa ajili ya wafugaji, linakabiliwa na uvamizi ambao ni tishio kwao kwa kuwa wanakosa malisho ya mifugo yao.

Sokoi Malimengi, mmoja wa wakazi wa kitongoji hicho, alisema wafugaji walipelekwa katika eneo hilo mwaka 2014 baada ya kufanyika Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi. Sasa kuna mabadiliko kutokana na uvamizi unaoendelea.

"Kuna mtu anajulikana kwa jina maarufu la Ken, anavamia maeneo ya wafugaji, anakata miti na watu wanashindwa kumsogelea kwa kuwa anakuwa na silaha za moto, hii ni hatari kwetu, tunakosa sehemu ya kulisha mifugo na makazi," alilalama.

Paulo Samnyesi, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema kuwa tangu uvamizi huo uanze, wametoa taarifa katika ofisi za kijiji, kata na wilaya lakini hakuna hatua zulizochukuliwa kutatua kero hiyo.

Aliomba Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa waingilie kati kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kabla hayajatokea madhara.

Lucas Kinani, mkazi wa eneo hilo, alidai kuwa kuna siku mtu huyo alifika na greda na kubomoa nyumba na zizi lake na baadaye alikata miti katika eneo hilo na hata walipotaka kuzungumza naye hakuwa tayari kuwasikiliza.

Kwa mujibu wa Morani Mbambaeai, Ken anamiliki zaidi ya ekari 2,000 ambazo mfugaji huyo anadai mtu huyo amezitwaa kwa nguvu kutoka kwa wananchi.

Wananchi hao pia waliomba watendaji wa serikali kuzuru katika eneo hilo ili kuona lilivyobadilishwa matumizi na ikiwezekana watengewe maeneo mengine kwa ajili ya makazi na mifugo yao, Hata bwawa walilokuwa wanalitumia wamezuiwa kulitumia.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi kwa simu, alisema malalamiko hayo hayajamfikia. Alitaka walalamikaji kuyafikisha ofisini ili yashughulikiwe.



Madiwani kutoka Halmashauri ya Msalala, wakijionea shamba la kilimo biashara linaloendeshwa na vijana katika kijiji cha Matongo, wilayani Tarime, mkoani Mara juzi. Shamba hilo, lilianzishwa kwa ufadhili wa mgodi wa North Mara kwa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Changamoto 21 kati ya 25 za Muungano zatatuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimetatua hoja 21 za Muungano kati ya 25 zilizokuwapo awali.

Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha mawaziri wa SJMT na SMZ cha

kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Nyamanzi, Zanzibar.

Alisema kuwa tangu mchakato wa kutatua changamoto hizo ulipoanza hadi sasa, zimebaki hoja nne za Muungano ambazo serikali zote mbili zinaendelea kuzitafutia ufumbuzi.

Dk. Jafo ambaye ni Mwenyekiti Mwenza wa kikao hicho alisema viongozi wa pande zote mbili za Muungano wamekaa pamoja kujadili hoja hizo nne zilizobaki na kuangalia namna ya kuzipatia ufumbuzi.

Alizitaja hoja nne zilizobaki ni pamoja na suala la sukari, usajili wa vyombo vya moto, Bodi ya Pamoja na Mgawanyo wa Mapato ya iliyokuwa Sarafu ya pamoja ya Afrika Mashariki.

Kutokana na mafanikio hayo, Dk. Jafo alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa wanayofanya katika kutatua hoja zilizobaki.

**Alisema kuwa tangu mchakato wa kutatua changamoto hizo ulipoanza hadi sasa, zimebaki hoja nne za Muungano ambazo serikali zote mbili zinaendelea kuzitafutia ufumbuzi.**

"Niwapongeze pia mawaziri, makatibu wakuu na wataalamu mbalimbali kutoka serikali za pande zote za Muungano kwa kuwa wamefanya kazi kubwa ya kuchakata changamoto zilizokuwapo hadi kufikia mafanikio haya," alisema Dk. Jafo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Hamza Hassan Juma alisema lengo la kikao hicho ni kuzungumzia hoja mbalimbali zinazokabili utendaji wa shughuli za SJMT na SMZ.

Alisema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umedumu kwa muda mrefu kutokana viongozi wa pande zote mbili za Muungano kukaa pamoja na kujadili changamoto zinazojitokeza kwa uwazi na kuzipatia ufumbuzi kwa pamoja.

Akitolea mfano wa mafanikio ya Muungano huo, Hamza alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inayoundwa na nchi nane inaendelea kudumu kutokana na uzoefu unaopatikana Tanzania na hivyo jumuiya hiyo kuendelea kukua.

Aliongeza kuwa hoja nyingi zimeshatatuliwa, hivyo mkutano huo unatoa matumaini makubwa kupatikana maslahi ya wananchi wa pande zote mbili pamoja na kuendelea kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao unatimiza miaka 60 ifikapo Aprili 26, mwaka huu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: CAPTAIN (30 POSTS)

**1.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons' equipment or above with a good performance.

**1.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
ii. Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
iii. Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
iv. Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
v. Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
vi. Report all incidents and accidents.
vii. Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
viii. Report any Flight delays of flights.
ix. Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
x. Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 2. POSITION: FIRST OFFICER (14 POSTS)

**2.1 MINIMUN ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must have flown with more than 250 flying hours or above with Commercial Pilot License, Multi Engine with Instrument Rating.
- Must be with an experience of handling a minimum of 10 tons' equipment with good performance.

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To participate in the Pilot-in-Command's crew briefing, and make himself aware of all relevant aeronautical and meteorological information as well as relevant papers documenting the aircraft technical status and its anticipated load.
ii. To prepare the OFP and when necessary, file the ATS Flight Plan with the appropriate Authority. If stored plans are used, then he should ensure that the correct plan has been activated
iii. To carry out such duties concerning the flight in accordance with the SOP, including procedures, limitations and performance related to the specific aircraft type, as allocated to him by the Pilot-in-Command;
iv. To confirm the safe navigation of the aircraft, maintaining a continuous and independent check upon both the geographical position of the aircraft and its safe terrain clearance
v. To safely and properly conduct the flight in compliance with the current flight plan and the Pilot-in-Command's instructions when the Pilot-in-Command is not at the controls. Any change to the current flight plan has to be notified to the Pilot-in Command.
vi. To provide advice, information and assistance to the Pilot-in-Command, as may contribute favorable towards the safe and efficient conduct of the flight.
vii. To assist the Pilot-in-Command in administration duties related to the flight and
viii. To seek and receive information and/or explanation from the Pilot-in Command, as may be necessary to enable fulfilment of functions.
ix. To assist the Flight Safety Department for all Technical related matters
x. Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 3. POSITION: SENIOR INTERNAL AUDITOR (1 POSTS)

**3.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:**

- Must be a holder of Bachelor Degree or Advanced Diploma in Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from recognized institutions plus CPA (T), ACCA, ACA, CIA or equivalent professional qualification recognized by the NBAA
- Must have working experience of at least seven (7) years in related field.
- Working experience in an aviation industry is an added advantage.
- Registration in ACPA-PP or equivalent registration will be an added advantage.
- Must be computer literate.

**3.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To prepare and arrange for contact with client and execute all required meetings for the allocated audit engagement.
ii. Review audit tentative programs, internal control and risk and engagement plan
iii. Administer and coordinate activities of the allocated audit engagement.
iv. Evaluate the adequacy and effectiveness of the controls in the audited areas.
v. Develop comprehensive practical programs and schedules for Audit coverage areas
vi. Review all documented audit findings and ensure their effective communication to the client and obtain responses.
vii. Prepare draft and final audit engagement reports.
viii. Schedule project and staff assignment to comply with the management needs with scope of the department over all schedules.
ix. Conduct special investigations as assigned by chief internal auditor/ other relevant authorities.
x. Coordinate audit schedules to avoid conflict with external auditor's work.
xi. Assist in preparation of annual budget and annual internal audit plan for the unit.
xii. To perform any other related duties as may be assigned by the supervisor.

## 4. POSITION: SALES AND MARKETING OFFICER I- TLO, CARGO & GROUND HANDLING (1 POST)

**4.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be a holder of Bachelor Degree in any field.
- The candidate must have one of the following certificate; Air Transport Management, Air Cargo, Dangerous Goods, Ground Handling, or equivalent qualifications from any recognized Aviation institution.
- Must have four (4) years working experience in related field (aviation field).
- Possession of two or more of the above professional certificates will be an added advantage.

**4.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Review of Ground handling services such as; check in, baggage sorting, passenger on transit, cargo handling & management.
ii. Review of ground handling contract performance as per existing contract and SLA.
iii. Review charge for excess baggage and report accordingly.
iv. Review issued tickets and miscellaneous charge order and airway bills.
v. Observe the arriving/departing passengers through control and to the transfer desk.
vi. Review handle acceptance of coffins, perishables and courier shipments.
vii. Physical verification of all Travel/Cargo agents and tour operators and submit sales visit report
viii. Review yearly Revenue Optimization strategy for assigned routes taking into account seasonal fluctuations.
ix. Review any fares/incentives that competitors offer to travel agents.
x. To perform any other related duties as may be assigned by the supervisor.

## 5. POSITION: SAFETY OFFICER II (ENVIROMENTAL) (1 POST)

**5.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be a holder of Bachelor degree in one of the following fields, Environmental Science and Management, Environmental Planning and Management, Geography and Environmental Studies, Environmental and Climatic Change or equivalent qualification from any recognised institution.

**5.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Initiate and coordinate implementation of environmental programmes aimed at reducing environmental impact to the community
ii. Coordinating the Company's activities regarding the development, implementation and maintenance of the Safety, Health and Environmental Program
iii. Recommending to the Head of Quality and Safety, Health and Environmental programs and policies to be developed and proposing amendments to such policies and programs where necessary
iv. Ensure ATCL participate to the global environmental sustainability programs such as CORSIA
v. Collecting, collating, and producing periodic Industrial Safety and Environmental reports and/or information so as to identify significant HSE trends for action by management to ensure compliance with ICAO Annex 16, Occupational Health & safety-OSHA, Environmental Management Act –EMA and ISO 14001 standard.
vi. Conducting HSE inspections and surveys of operational systems, infrastructure and procedures affecting or likely to affect the company operations and assess risk exposure.
vii. Following up and verification of implementation of the HSE recommendations developed by the Health, Safety and Environmental Committee's (HSE) to continuously improve and maintain safety and environmental protection.
viii. Promoting a culture within the company to raise the level of safety and environmental awareness as well as oversee the recycling of products from ATCL operations to generate revenue out of waste products.
ix. Investigating workplace, ground and environmental incidents/accidents and make appropriate corrective/preventive recommendations to the relevant/affected department/sections while assisting the Responsible Managers achieve effective implementation of the recommended actions.
x. Preparation, production, and dissemination of HSE information bulletin to raise health, safety and environmental awareness.
xi. Conducting periodic ground and workplace HSE audits for company and third party organizations to assure compliance with company policy and requirements as well as industry for management decision.
xii. Ensuring effective and appropriate communication and coordination with relevant regulatory Authorities, customer airlines, contractors over matters concerning Industrial Safety and Environment with a view to agreeing on solutions common concerns.
xiii. Facilitating meetings for Health, Safety and Environmental Committees and ensure that such meetings are held as per schedule.

## 6. POSITION: AIRCRAFT MAINTENANCE ENGINEER II- 5 POSTS

**6.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be holder of diploma in Aircraft Maintenance Engineering with Aircraft Maintenance Engineers License (AMEL) without type rating.
- Possession of Bachelor Degree in Aeronautics / Bachelor Degree in relevant engineering field from a recognized institution or its equivalent is an added advantage.

**6.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Assist in removal and installation of aircraft components, repair, assembling and testing of aircraft systems.
ii. Assist in repair, test, overhaul and calibration of equipment and tools as per approved procedure.
iii. Supervise Aircraft Technicians in a particular field.
iv. Performs any other official duties as may be assigned by the supervisor.

## 7. POSITION: PLANNING & DEVELOPMENT ENGINEER II (15 POSTS)

**7.1. MINIMUN ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be a holder of Bachelor Degree in Aeronautical Engineering or equivalent qualifications from a recognized institution and
- Must have a knowledge on Aircraft System or Workshop.

**7.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Assist in planning aircraft check dates according to check intervals and aircraft utilization.
ii. Assist in preparing check packages for aircraft

# 'Wananchi ombeni maeneo yenu ya ardhi yatambuliwe'

**Na Munir Shemweta,** MBULU

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ametaka wananchi wilayani Mbulu, mkoani Manyara kujitokeza kwa wingi kuomba maeneo yao ya ardhi kutambuliwa.

"Ninaomba mwendelee kujitokeza kwa wingi ili maeneo yenu yatambuliwe na hii itasaidia sana wananchi wa M bulu kutogombana katika masuala ya ardhi kwa kuwa kila mmoja atakuwa na hati yake," amesema.

Naibu Waziri Pinda alitoa kauli hiyo juzi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu wakati wa kutoa hati kwa wananchi waliotambuliwa kupitia mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) akiwa katika ziara yake ya siku mbili mkoani Manyara.

Jumla ya wamiliki wa ardhi 68 katika Wilaya ya Mbulu walikabidhiwa hati milki za ardhi zilizopatikana kupitia mradi huo.

"Kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo yenu hakumnyang'anyi haki mwenye eneo na kinachofanyika ni kutambua eneo lako, kama ni shamba lako litambuliwe na kama ni kiwanja kitambulike," alifafanua.

Naibu Waziri huyo alipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kutokana na wilaya hiyo kutokuwa na migogoro mikubwa ya ardhi na kubainisha kuwa iwapo maeneo yote ya wilaya hiyo yatapimwa, migogoro ya ardhi itakwisha.

Vilevile, Naibu Waziri huyo alihimiza wananchi wa Mbulu kuchangamkia hati zinazotolewa kupitia mradi wa KKK huku akiagiza Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Manyara kuhakikisha inahamasisha wananchi kujua ubora na matumizi ya hati.

"Tunataka kuhakikisha Mji wa Mbulu unapangwa vizuri na kuwa katika mandhari nzuri," alitamba Naibu Waziri Pinda.

Vilevile, kiongozi huyo alisema kuwapo kliniki za ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini ni sehemu ya juhudi za wizara yake kushughulikia migogoro ya ardhi.

Aliagiza Msajili wa Hati na Nyaraka Mkoa wa Manyara kuhakikisha anaharakisha utoaji hati kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ili kuwaondolea usumbufu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Kheri James alipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kupeleka mradi wa KKK ndani ya wilaya yake mradi, akiutaja umesaidia maeneo ya wilaya hiyo kupangwa, kupimwa na kumilikishwa.

"Mpango wa upimaji na upangaji katika wilaya yetu umetufanya tuzuru kila kijiji na kata kuelimisha, kukumbusha na kuhamamisha wananchi," alisema James.



Meneja Mkuu wa Veltex, Herbert Swai, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu utalii tiba unaoratibiwa na taasisi hiyo wa kupokea wagonjwa kutoka nchi mbalimbali na kuwaunganisha na madaktari wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa ajili ya matibabu. **PICHA: MPIAGAPICHA WETU**

# Maboresho miundombinu afya yachochea tiba utalii

**Na Latifa Abdallah**

TAASISI ya Vertex imeipongeza serikali kwa kuimarisha tiba utalii inayoitangaza nchi duniani baada ya kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika hospitali nchini.

Uongozi wa taasisi hiyo umesema tiba utalii inasaidia kutangaza nchi kimatibabu kwa wagonjwa wanaokuja kutibiwa nchini chini ya uratibu wa tasisisi hiyo kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Meneja Mkuu wa Veltex, Herbert Swai, alitoa pongezi hizo kwa serikali juzi jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari na wagonjwa raia wa Morocco waliopata matibabu nchini kupitia uratibu wa taasisi hiyo.

Alisema miundombinu iliyojengwa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya imekuwa kivutio kwa wageni kuja nchini, hivyo kuongeza idadi ya watalii, pia fedha za kigeni.

"Sisi Vertex tunasaidia kuratibu utaratibu wote wa mgonjwa kuanzia anapotoka kwenye nchi yake mpaka anapata huduma zote za matibabu katika hospitali za nchini pasipo kupata usumbufu wowote pindi anapofika hospitalini," alisema.

Swai alibainisha kuwa kwa mwaka 2023, waliratibu huduma hizo kwa wagonjwa 47 kutoka nchi mbalimbali, akitoa rai kwa wananchi wote nchini kutumia huduma hiyo kwa kuwa tiba utalii si kwa ajili ya wageni pekee, bali pia kwa wazawa. "Tiba utalii ni ya wote.

Watanzania nao wanapaswa kuitumia kwani nchi yetu imejipanga vizuri. Kuna vifaa vya kisasa, pia kuna madaktari wabobezi, hivyo niwashauri Watanzania kuja Vertex ili tuwasaidie kuwaunganisha na madaktari bila kupata usumbufu wowote ikiwamo foleni hospitalini," alisema.

Nasra Samadani, Mwanasheria wa Vertex alisema kuwa mpaka sasa wana mkataba na Hospitali ya Taifa Muhimbili na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na wamejipanga kufikia hospitali nyingi zaidi nchini.

Alisema licha ya mafanikio hayo, wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo namna ya kuwafikia wagonjwa wengi zaidi waliomo ndani ya nchi na upungufu wa fedha kwa ajili ya kutoa elimu zaidi.

Samadani alitoa rai kwa wageni na wenyeji kuepuka madalali, badala yake watumie taasisi hiyo kwa ajili ya kupata huduma bora na zenye uhakika kutoka kwa madaktari wabobezi nchini.


iii. Assist in compiling and updating aircraft maintenance and component life
iv. Assist in preparation and issuing of daily May Fly, showing aircraft movement and their details.
v. Assist in developing and design modifications to structure, power plants, landing gears components and systems.
vi. Assist in conducting periodic salvage investigation.
vii. Performing any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**8. POSITION: GROUND SUPPORT TECHNICIAN II (3 POSTS)**

**8.1 MINIMUN ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be holder of Form IV Certificate with Professional Level III in one of the following fields; Motor Vehicle Mechanics, Truck Mechanics, Auto Body Repair, Diesel Engine Mechanics, Heavy Duty Equipment Mechanics, Auto Electrical, Motor Cycle Mechanics, Plant Operator or its equivalent qualification from recognized institutions.

**8.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To assist in carrying out minor repair jobs on ground support equipment.
ii. To assist in maintenance of company vehicles.
iii. Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**9. POSITION: AIRCRAFT CLEANER II (5 POSTS)**

**9.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must have Form IV Certificate with two pass in any subjects,
- Must have any relevant Certificate from VETA or any recognized institutions.
- He/she will attend In- house training in the following fields; ATCL Maintenance procedures, aircraft, component, hangar facilities, working safety gears and cleaning.

**9.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Handle general cleaning of line, hangar and workshop facilities under supervision
ii. Clean Aircraft and aircraft components under supervision.
iii. Assist in positioning working and safety gears to facilitate maintenance activities.
iv. Performs any other duties as may be assigned by the supervisor

**10. POSITION: SAFETY OFFICER II (1 POST) (READVARTISEMENT)**

**10.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS**

- Must be holder of any Bachelor degree preferably Bachelor Degree in Science or ATPL or Flight Operations License or equivalent qualifications from recognized Institutions.
- Training in Quality Management System and/or safety management systems from a reputable organization shall be added advantage.

**10.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Monitor status of Company Safety and emergency equipment's under supervision.
ii. Assist in monitoring through safety audit status of airports network.
iii. Carry out regular inspections of Company premises to identify issues that affect ground and flight safety.
iv. Prepare annual quality assurance program that provides for the auditing of the management system of operations, and maintenance functions.
v. Ensure equipment and operational products that are purchased or otherwise acquired from an external vendor or supplier meet the product technical requirements specified by the company prior to being used in the conduct of operations or aircraft maintenance.
vi. Ensure conformity with ICAO requirements by coordinating initial and renewal audits to air operators that transport company passengers under a commercial aviation agreement.
vii. Make follow up on findings that result from audits conducted under the quality assurance program by ensuring identification of root cause, development of corrective action appropriate to address findings, implementation of corrective action in appropriate operational area(s) and evaluation of corrective action to determine effectiveness.
viii. Prepare and coordinate the communication and coordination with operational managers in the management of operational risk.
ix. Prepare audit plan with sufficient resources and scheduled audits at intervals that meet regulatory and management system requirements including ensuring that are conducted within the scheduled interval.
x. Prepare and Maintain an electronic database for audits conducted under the quality assurance program
xi. Perform any other official duty as may be assigned by your supervisor.

**11. TERMS AND CONDITIONS:**

Ten (10) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**12. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.


**13. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**

ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.

**Date: 7th March, 2024**



# Milioni 33/- zatumika ujenzi matundu ya vyoo sekondari

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHULE ya Sekondari Busiya iliyopo wilayani Kishapu mkoani hapa ambayo ilikuwa ikikabiliwa na uhaba wa vyoo, imepata msaada wa kujengewa matundu 12 pamoja na chumba maalumu kwa ajili ya wanafunzi wa kike kujisitiri wakati wa hedhi.

Shule hiyo yenye wanafunzi 351 (wavulana 176, wasichana 175) awali walikuwa wakitumia matundu sita ya vyoo pasipo kuwa na chumba maalumu cha kujisitiri kwa ajili ya watoto wa kike, hali iliyokuwa ikisababisha utoro wa mara kwa mara.

Msaada wa ujenzi wa matundu hayo na chumba maalumu cha kujisitiri ulitolewa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Shinyanga.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya benki hiyo kukamilisha na kukabidhi majengo hayo, wanafunzi hao walisema uwepo wa vyoo na chumba hicho maalumu kutasaidia kupunguza utoro hasa nyakazi za hedhi.

Dada Mkuu wa shule hiyo, Mary Richard alisema: "Wakati wa hedhi tulikuwa tunasitisha masomo kutokana na shule kutokuwa na eneo maalumu kwa ajili ya kujisitiri, hivyo utoro huo wa mara kwa mara ulikuwa ukishusha ufaulu hasa kwa wanafunzi wa kike".

Mwanafunzi mwingine Joseph Masanja, alisema uhaba wa vyoo shuleni hapo ulihatarisha afya zao kutokana na wanafunzi kujisaidia ovyo vichakani na baadaye kuhatarisha afya zao wakati wa mvua.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Busiya, Badi Mfinanga, alisema hali hiyo itainua ufaulu kutokana na utoro kupungua na kubadili matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana aliyoyataja kutokuwa ya kuridhisha.

Meneja wa Benki ya TCB Tawi la Shinyanga, Julius Mataso, alisema walibaini matatizo katika shule hiyo alipoalikwa mgeni rasmi katika mahafari ya kidato cha nne.

"Hivyo ikabidi kutoa sehemu ya faida yetu ambayo huwa tunaipata na kuirudisha kwa jamii, kuwajengea vyoo bora viwili vyenye matundu 12, na chumba maalumu cha kujisitiri hedhi ambavyo kwa pamoja viligharimu Sh.milioni 33.7," alisema Mataso.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, David Mashauri, alisema kwa shule za sekondari bado kuna upungufu wa matundu ya vyoo 246.

Alisema uhitaji ni matundu 520, kwamba yaliyopo 274 na kuwa serikali imetoa Sh.milioni 75 kujenga matundu mengine 75 na kupunguza upungufu uliopo.



Mkuu wa Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, Rachel Kassanda (kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wanufaika wa mafunzo ya ujasiriamali na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa wanawake yaliyodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vyama 8 kushiriki uchaguzi mdogo wa udiwani Sengerema

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

VYAMA vinane vya siasa vimeteuliwa kusimamisha wagombea udiwani katika uchaguzi mdogo wa diwani katika Kata ya Buzilasoga Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza

Vyama hivyo ni pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM), National League for Democracy (NLD), United Peoples' Democratic Party (UPDP), Sauti ya Umma (SAU), Chama cha Wakulima (AAFP), Chama cha Kijamii (CCK), Demokrasia Makini na TLP.

Akitangaza matokeo ya uteuzi huo, Ofisa Msimamizi Msaidizi wa Uchanguzi Kata ya Buzilasoga, Benson Mpanju alisema jumla ya vyama 10 viliomba kuwa na wagombea lakini hadi kufikia Machi 4 mwaka huu saa 10.00 jion jumla ya vyama tisa kati ya 10 vilirejesha fomu na kati yao wagombea nane walikidhi vingezo.

Aidha alimtaja mgombea wa TLP, Benjamin Alexander kuwa hakuteuliwa kutokana na kutotimiza idadi ya wadhamini pamoja na kutolipa fedha ya dhamana.

Alisema wagombea waliotheuliwa ni pamoja na Edina Godwin Bandihai (CCM), Deus Kabilondo Nkwabi (NLD), Ramadhan Omary Said (UPDP), Saida Ramadhan Abdul (SAU), Rehema Hussein Khery (AAFP), Anna Sulwa Zengo (CCK), Msafiri Joseph Nyamwitanga (Demokrasia Makini).

Aidha alisema baada ya wagombea hao kuteuliwa umetolewa muda wa pingamizi ndani ya saa 24 uliotamatika Machi 5, saa 10.00 jioni.

Alisema baada ya hapo kampeni za uchaguzi mdogo zimeanza Machi 5 hadi 19 mwaka huu na uchaguzi huo utafanyika Machi 20 ili kuziba nafasi hiyo kufuatia kifo cha aliyekuwa diwani wa kata hiyo, David Shilinde.

# DC ahimiza ulinzi mradi wa maji vitongoji vitano

**Na Neema Emmanuel,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu, Rachel Kassanda, amewataka wananchi kuimarisha ulinzi na kutunza Mradi wa Huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Usafi (WASH), ili kuunga mkono mipango ya serikali ya kuimarisha upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo ya vijijini.

Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi 11,927 katika vitongoji vitano vya Ilambu, Mlimani, Igogo, Shuleni na Majengo.

Kassanda alitoa kauli hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa bonanza la WASH lililofanyika wilayani hapa ambalo liliandaliwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti kwa kishirikiana na Africa Community Advancement Initiative (AFRIcai) inayojihusisha na afya, elimu, maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii mbalimbali za kitanzania.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi katika kuwawezesha wanawake kutoka maeneo vijijini, ili kutatua changamoto wanazokabiliana nazo ili kujikimu kimaisha na kuhakikisha uendelevu wa vizazi vijavyo.

"Napongeza juhudi za ushirikiano za SBL na serikali, kwani ni faida kwa sekta zote mbili, ushirikiano unaohakisi umuhimu wa kuwawezesha wanawake katika maeneo ya vijijini kupitia mipango kama hiyo,"alisema.

Kassanda alisema katika kila jumuiya ambapo SBL inatekeleza miradi ya WASH, kamati zinaundwa zenye uwakilishi sawa kutoka kwa wanaume na wanawake, ikikuza fursa za maamuzi jumuishi na uendelevu wa muda mrefu.

Meneja Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu, alisema lengo la bonanza hilo ni kukuza uwiano wa kijamii na ushirikiano wa jamii, sambamba na kutambua mchango wa vikundi vya wanawake katika kuhakikisha umiliki wa mradi wa WASH unakuwa endelevu.

"Mradi huu unafanywa kwa ushirikiano na Africa Community Advancement Initiative (AFRIcai), inayojihusisha na afya, elimu, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii mbalimbali za kitanzania. Ushirikiano huu wa kimkakati unalenga kuondoa uhaba wa maji kwa kuwapatia majisafi na salama wananchi 11,927 katika vitongoji vitano vya Ilambu, Mlimani, Igogo, Shuleni na Majengo," alisema.

Alisema katika kuhakikisha uendelevu wa miradi hiyo, SBL na AFRICAi waliendesha programu maalumu ya mafunzo ya siku mbili ambapo wanawake 25 waliwezeshwa ujuzi na maarifa muhimu katika masuala mbalimbali ya shughuli za WASH, ujasiriamali, usimamizi wa fedha, usafi wa kimasoko, mazingira, na kukuza jitihada za usafi.



Ukurasa 12
KUELEKEA MKUTANO KIMATAIFA ECD...
**Utafiti na darasa kamili la malezi, kasoro zilikojificha**



Ukurasa 13
Ummy atia mguu Lindi, wakiwekana sawa hali Ukimwi, upatikanaji dawa



Ukurasa 14
JANGA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA...
**Serikali inaandaa kampeni michezo ya rede, kuruka kamba viwanja vya shule**

AFYA

SIMULIZI OFA AFYA JIMBONI...

# Siku Waziri Ummy akawa mwenyeji mtoaji 'ahsante afya' kwa Rais wake

• Atamba; vyote Bombo, hakuna safari Dar, wala Moshi

**Na Mwandishi Wetu**



Mandhari ya Hospitali ya Rufani ya Bombo, jijini Tanga, ambayo imefanyiwa maboresho makubwa. **PICHA: MTANDAO**

MARA zote, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, kazoeleka katika kazi yake kunadi 'ahsante' ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kufikisha huduma za afya mahali mbalimbali.

Lakini tarehe 22 mwezi uliopita, ilikuwa tofauti, Waziri Ummy akaonekana mwenyeji wa 'ahsante' hiyo akiwa jimboni kwake na ugeni mkubwa, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango. Hapo akafunua siri, Rais kawatengea fedha shilingi bilioni 25 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji maji safi na salama jijini Tanga na maeneo pembezoni, ambako Ummy ndiye mwakilishi wao bungeni.

Hiyo ilikuwa katika hafla ya kuzinduliwa Hati Fungani ya Kijani ya miundombinu ya maji mkoani Tanga, ambayo Ummy hakuficha hisia zao kumpa maua yake Rais Dk. Samia, kwa ajili ya kuwatatulia kero zao, akiorodhesha; elimu, afya, barabara na maboresho ya Bandari Tanga.

Hapo ndipo akarejea ya ofisini kwake, akisema jiji la Tanga lina vituo sita vya afya ambavyo vinafanya kazi, akiwa na ufafanuzi:

"Kwa upande wa Hospitali za Rufani, tumesambaza mashine za kisasa za uchunguzi ikiwamo 'CT-Scan' katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Rufani ya Bombo Tanga."

Anasema hiyo inawaondolea ulazima wananchi wa Tanga sasa kwenda tena Dar es Salaam au mkoani Kilimanjaro kufuata huduma za 'CT-Scan' au huduma za kusafisha damu, kwani zote zinapatikana mkoani kwao.

"Hatua hii ni kubwa ambayo Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anafanya ya kuwajali wananchi wake na anaendelea sasa kwenye sekta ya maji.

"Rais Samia atatupatia shilingi bilioni 53 kwa ajili ya mradi wa upatikanaji wa maji kwa asilimia 100 kwa wakazi wa Tanga Mjini pamoja na wilaya jirani za Muheza na Mkinga," anajinasibu Ummy, mbele ya msaidizi mkuu wa Rais Dk. Samia.

Mradi wa maji uliozinduliwa Tanga unatarajiwa kuzalisha wastani wa lita milioni 60 kutoka lita 45 za awali mkoani Tanga.

Ni aina ya kicheko hicho mkoani Dar es Salaam, mwezi kabla ya kilichofanyika Tanga, illikuwa Januari 11, kongole nayo kwa Rais Dk. Samia, akiwekeza katika sekta ya afya hususani huduma ya 'Mama na Mtoto' lengo ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pingamizi.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, aliwakabidhi wabunge wa majimbo 10 ya mkoa wa Dar es Salaam, vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 691, vilovyotolewa na serikali kwa majimbo hayo.

Chalamila anasema, ni miongoni mwa vifaa vilivyozinduliwa wiki moja kabla na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kwa ajili ya nchi nzima vikiwa na gharama ya shilingi bilioni 14.9. Akaeleza kuwa uwekezaji huo unaofanywa na serikali katika sekta ya afya, umeleta mapinduzi makubwa ya utoaji huduma hivyo anatoa wito kwa jamii kuchangamkia fursa ya bima ya afya kwa wote, ili kupunguza gharama za kijitibu.

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Mavere Tukai, anasema serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 14.9 kununua vifaa hivi kwa ajili ya nchi nzima na MSD ndiyo imenunua na itavisambaza kwa majimbo hayo 214 nchi nzima.

Anasema mkakati wa kugawa vifaa hivyo ulizinduliwa na Waziri wa Afya, Ummy ambao serikali imetumia shilingi bilioni 14 kununua vifaa hivyo ambavyo vitasambazwa katika halmashauri za wilaya zote nchini.

Kwa mujibu wa Tukai, kwa Dar es Salaam vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 700 vitagawiwa katika zahanati na vituko vya afya vyote mkoani humo.

AFYA

## KUELEKEA MKUTANO KIMATAIFA ECD...

# Utafiti na darasa kamili la malezi, kasoro zilikojificha



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Babati, wakiwa katika Uwanja wa Kwaraa, wakiwasikiliza viongozi wa serikali. **PICHA: JALIWASON JAS-**

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

TANZANIA imo katika nchi za kwanza Afrika, kuanzisha Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), ikifanya uchechemuzi kumsaidia mtoto akue kwa utimilifu, kufika miaka nane.

Hapo kuna afya, kujifunza elimu ya awali, lishe bora, ulinzi na usalama na malezi yenye mwitikio.

Utafiti wa kitaasisi wa Tanzania Demographic Health Survey (TDHS-MIS) mwaka 2022, una ufafanuzi wake. PJT-MMMAM ilizinduliwa nchini Desemba 13, 2021 na aliyekuwa Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

### WADAU WAUCHAMBUA

Mkurugenzi wa Shirika la Children Incrossfire (CIC), Craig Ferla, anasema kiashiria ni cha Malengo Maendeleo Endelevu (SDG) 2030 katika mwelekeo wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kufikia mwaka 2030, yamegusa afua tatu.

Anazitaja kuwa; afya, ujifunzaji wa awali unaoangalia lugha ya mtoto kujieleza, kujifunza kuandika na kuhesabu na saikolojia yake, ikigusa hisia za mtoto, kuchangamana na kujifunza tabia.

Mkurugenzi anasema, SDG inataja hatua za ukuaji wanazopitia watoto; miezi 24 hadi 29, akikidhi vigezo saba vya ukuaji na miezi 30-35 akitakiwa walau kutimiza vigezo tisa vya ukuaji.

Mtoto wa miezi 36-42, anatakiwa kutimiza vigezo 11 vya ukuaji. Ferla anasema, ripoti inaonyesha mtoto wa miezi 48-59 anapaswa kuwa na vigezo 15 vya ukuaji.

Anasema, TDHS-MIS ya 2022 inaeleza asilimia 47 ya watoto nchini, wako kwenye mwelekeo sahihi na asilimia 53 ya hawako kwenye mwelekeo sahihi.

> “Naamini kabisa, magari haya yatatumika katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa ‘TB’ kwa kuibua wagonjwa wapya, mapambano dhidi ya malaria na ukimwi.

Mkurugenzi huyo anashauri wazazi kuwekeza siku 1000 za awali za mtoto, zikiwa na msisitizo kwenye ukuaji wa mtoto.

Anafafanua wanapowekeza kwenye siku 1000 mtoto atakua vizuri, hasa wakati huo ikiwa ni miaka miwili mpaka mitatu, ubongo wake ndio unakua kwa kasi zaidi.

Mtaalamu huyo wa malezi na makuzi, anasema watoto wenye miezi 36 mpaka 47, mwelekeo wa ukuaji sahihi wao unapungua kutoka asilimia 58 na kushuka mpaka asilimia 45, huku wenye miezi 48 hadi 59, ukuaji wao sahihi unapungua hadi asilimia 36.

Mkurugenzi anasema, watoto wa mjini hufuatiliwa au wako kwenye mwelekeo sahihi na utafiti unaonyesha asilimia 56, huku wa vijijini, wanaofuatiliwa ni asilimia 44 pekee.

Mbobezi huyo anaeleza Zanzibar, utafiti unaonyesha asilimia 60 ya watoto walio kwenye mwelekeo; Kanda Magharibi 20.6%; Kusini 25.9%; Kusini Magharibi 30.7%; Kaskazini 60%; Kanda Kati 56%.

Ferla anasema, THDS-MIS 2022 inafafanua kinamama wasio na elimu, walio na watoto kwenye mwelekeo sahihi 32% na waliomaliza sekondari, 61% ya watoto wao wako kwenye mwelekeo sahihi.

Pia anasema 36% ni kaya zisizokuwa na uwezo na ndio zipo kwenye mwelekeo sahihi, kaya zenye uwezo mkubwa ni 65% ya watoto wao nao wako kwenye mwelekeo sahihi.

Vilevile anasema, 27% ya Watanzania walikuwa na umri wa malezi na makuzi, umri miaka minane au pungufu, na idadi ya Watanzania milioni 16 kwa mujibu wa Ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022.

Ferla anasema, fursa ya kuwekeza kwa watoto ili wawe na tija kuanzia ngazi ya familia hadi taifa, haijirudii, kama wazazi hawatachukua hatua.

Utafiti wa TDHS-MIS wa 2022, watoto walioko kwenye mwelekeo sahihi, kwa mikoa Arusha ni asilimia 73.1; Kilimanjaro 69.8; Kagera 69.0; Iringa 68.2; Njombe 65.0, Dodoma 61.3; Mbeya 52.6; Mara 56.4; Singida 54.8; na Simiyu 51.8.

Mikoa mingine, Dar es Salaam asilimia 51.4; Manyara 50.0; Pwani 48.8; Mwanza 48.2; Geita 47.9; Tanga 46.6; Morogoro 45.8; Shinyanga 45.4; Mtwara 29.1; Katavi 27.8; Songwe 24.8; Kigoma 21.7; Ruvuma 22.9; Lindi 21.5; Tabora 20.3 na Rukwa 16.0.

Mdau wa Malezi, Alinune Nsemwa, anashauri jamii kuacha kumpa mtoto chakula cha aina moja, akieleza kuna wakati wazazi wanakosa muda kuwapatia chakula.

Anawataka sasa kuwachangamsha watoto, jambo linalotakiwa, akishauri serikali iweke kipaumbele kutenga bajeti ya lishe na kujifunza. Ni vizuri kuwekeza kwa mtoto kuanzia nyumbani na mtoto aliko.

Nsemwa, anafafanua tatizo la wazazi, kuwapo mtoto asipoenda shule, hawaoni umuhimu wa kucheza nao. Analalamika serikali kutenga bajeti kubwa vyuoni, kuliko madarasa ya awali penye umuhimu, akitoa mfano kuwapo nchi zilizoendelea kuna bajeti kubwa kwa watoto wa miaka kuanzia minane kushuka chini.

### KUELEKEA MKUTANONI

Nsemwa anasema, kuelekea Mkutano Kimataifa wa Afrika Mashariki wa Malezi na Makuzi ya Watoto, utakaoanza Machi 11 nchini, wataalamu watapata muda kubadilishana uzoefu wa suala hilo.

Pia Mkurugenzi wa Mradi wa Kuhudumia Watoto kutoka Shirika la Christian Social Services Commission na daktari bingwa wa watoto, Theopista Masenge, anasema utafiti wa TDHS-MIS 2022 uliangalia watoto kuanzia wenye miezi 24-59.

Anasema utafiti unatazama afya, mafunzo ya awali, wakimwangalia mtoto kujua, kuandika, kuhesabu na mchangamano na wenzao.

Dk. Masenge anasema, utafiti unaonyesha asilimia 47 ya watoto waliokuwa na ukuaji timilifu na waliobakia asilimia 53, hawakufikia hatua hiyo.

“Wanakuwa wazito hawawezi kujibu haraka ukiwauliza kitu au hesabu ndogo,” anasema Dk. Masenge.

Bingwa huyo anafafanua, mtoto anavyokua ndio wazazi na walezi wanampotezea malengo au ndoto zake, kutokana na kutokumlea kwa utimilifu.

Anashauri, mbinu mbadala wa kulea mtoto vinawasaidia kulinda kasoro zake mtoto, akitaja wanaochelewa kukaa, wazazi wanatakiwa kuwafuatilia wasaidiwe, kabla tatizo halijawa kubwa.

Mtaalamu huyo anaasa, watendaji wanatakiwa kuwezeshwa kutoa huduma na wananchi nao wanadai haki za mtoto.

“Mzazi anayemnyima mtoto haki ya kupata huduma ya afya hilo ni kosa la jinai kisheria anatakiwa kuchukuliwa hatua,” anasema, akitaja kuwapo sera kiserikali katika eneo hilo, lakini wazazi wengi hawazijui haki hizo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la EngenderHealth Tanzania, daktari mwandamizi wa magonjwa ya kinamama, Moke Magoma, anasema afya ya mama na mtoto haitegemei sekta ya afya pekee, bali mjumuiko wa kisekta kama maji, nishati na miundombinu.

Anatumia mfano, mjamzito anahudumiwa vizuri na mtoto wake, kwa msaada wa umeme, maji na barabara. Dk. Magoma anasema, kupungua vifo vya kinamama, kama utafiti wa TDHS-MIS wa 2022, sekta ya afya inatakiwa kuwa na watumishi wenye weledi na kuhakikisha kinamama wanapata huduma bora.

Anasema vifo vya kinamama kupungua maradufu ni zao la juhudi za kufuta vifo hivyo, kabla na baada ya kujifungua.

Anashauri kuendelea kuhimizwa uzazi wa mpango, ili mama awe na nafasi ya kulea mtoto kabla ya kupata ujauzito mwingine, akijiepusha na madhara.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Dareda Misheni inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Dk. Joseph Lorri, anaungana na utafiti wa TDHS-MIS 2022, inayotaja kuwa vifo vya kinamama wajawazito vimepungua, pia kwa watoto wachanga.

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Ummy atia mguu Lindi, wakiwekana sawa hali Ukimwi, upatikanaji dawa

**Na Yasmine Protace**

## • Wapeana mpango mbadala staili kuajiri

ELIMU ambayo imekuwa ikitolewa na serikali juu ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi, sasa inatajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa watu kujitambua afya zao.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwa ziarani kikazi mkoani Lindi, anasema kwa wanaogundulika na ugonjwa huo, wanapatiwa elimu ya kujitunza kiafya na kupatiwa matibabu kuwaweka ili wasipate maambukizi mapya.

Majarida,vipeperushi na maigizo juu ya ugonjwa huo nchini yanatolewa katika matamasha ya Siku ya Ukimwi Duniani, na walio na ugonjwa wanafika katika vituo vya afya kupata dawa sahihi, ambao hawajaanza dawa wanapatiwa elimu ya kujitunza wasipate maambukizi mapya. Ummy anazungumza kutoka ziarani mkoani Lindi, akisema maambukizi hayo mkoani humo yameshuka kutoka asilimia mbili hadi 1.7 mwaka jana.

Anaongeza kuwa takwimu hizo zimefanya kufikiwa malengo ya 95-95-95 mkoani humo, akisema viongozi wa mkoa wametakiwa kutobweteka na mafanikio, waendelee kuchukua hatua za elimu, ikiwa ndio mkombozi wa jamii.

Waziri Ummy ziarani akatembelea vituo vya afya Mnazi Mmoja na Mjini, Zahanati ya Nachingwea na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi.

"Niwapongeze Mkoa wa Lindi mmefikia malengo ya 95-95-95 ambayo asilimia 96 ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi, wanajua kwamba wana maambukizi.



Waziri Ummy Mwalimu, akiwa katika ziara ya kikazi kutembelea wagonjwa wodini, mkoani Lindi wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

"Asilimia 95 ya watu wenye maambukizi wapo kwenye dawa na katika asilimia hiyo 95 ya wanaotumia dawa, virusi vimefubazwa," anasema.

Ummy anawaasa wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha, ikiwamo kufanya mazoezi, ulaji vyakula kwa kupunguza chumvi, sukari na mafuta mengi kuepuka magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo kisukari.

**HALMASHAURI NA YAKE**

Waziri Ummy anazisisitiza halmashauri ikiwamo ya Wilaya ya Kilwa kuajiri watumishi wa mikataba, ikitumia mapato ya ndani, hata kupunguza changamoto za uhaba wa wataalamu wa afya katika wilaya hizo.

Ni kauli yake baada ya kupokea taarifa ya Hali ya Afya katika Halmashauri ya wilaya, hiyo iliyotolewa na Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Lusajo Mwakajoka.

Taarifa inaonyesha hali ya upatikanaji wa huduma za afya mkoani Lindi, upatikanaji wa vifaa tiba, pamoja na changamoto zake.

"Tutatumia njia kuu tatu, ili kupunguza changamoto za watumishi, ikiwa ni pamoja na njia ya vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais Utumishi.

"Tunaajiri watumishi kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, pamoja na wadau wetu wa maendeleo katika sekta ya afya nao wanaajiri ajira za mikataba pamoja." anasema.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack anamshukuru Waziri wa Afya, akimwomba kipaumbele, kwa kuwa kuna wananchi wengi wa kipato cha chini wanashindwa kufuata huduma mbali na makazi yao.

"Vifaa tiba zikiwamo dawa zinaposambazwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), tunaomba wawe wanawahi kwa wakati kwa kuwa wananchi wengi wa mkoa wa Lindi wana kipato cha chini.

"Dawa zinapochelewa tunamkwamisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa ameshatoa fedha za dawa, kikubwa ni sisi watendaji," aasema Waziri Ummy.

Anazitaka hospitali, vituo vya afya na zahanati kufanya maotea (makadirio) sahihi ya dawa, akisema ndio zitatoa usumbufu wa wananchi kupata huduma sahihi.

"Tunaposema dawa zipo, hatumaanishi dawa zote ziwepo, bali tunamaanisha kuwapo na makundi ya dawa ambazo zinapaswa kuwapo katika vituo husika. Sio kila dawa itapatikana katika kituo cha afya," anafafanua Ummy.

Anasema miongoni mwa makundi ya dawa yanayopaswa kuwepo katika vituo vya afya ni za kuzuia maumivu, zinazotibu maambukizi ya bakteria, dawa za watoto kama za kuharisha, vipimo vya haraka vya malaria, dawa za uzazi salama, presha na kisukari.

"Hali ya upatikanaji wa dawa katika Mkoa wa Lindi inaridhisha na nataka kusisitiza kipimo cha haraka cha malaria (MRDT) ni bure.

"Dawa ya kutibu malaria (Alu) ni bure, sindano ya kutibu malaria kali ni bure, dawa kwa ajili ya kutibu maambukizi ya bakteria kwa watoto nayo ni bure." anasema.

# Utafiti na darasa kamili la malezi, kasoro zilikojificha

**INATOKA UK.12**

Dk. Lorri anasema ni zao la kuboreshwa huduma za afya, kuajiriwa wataalamu wa kutolewa huduma bora.

Anagusia ujenzi wa vituo vingi vya afya na kuanzishwa kwa kitengo cha kufuatilia vifo vya watoto na wajawazito kutoka Wizara ya Afya na kufanyika mikutano mtandaoni na wataalamu wa afya kila mwezi imesaidia.

**OFISA MAENDELEO**

Ofisa Maendeleo Mkoa wa Manyara, Anna Fisoo, anasema utakuwa wa manufaa kitaifa, kukiwekezwa kwenye malezi na makuzi, ikisaidia kuunda taifa imara.

Fisoo anasema haja ya kuimarisha utoaji elimu, ili watoto wakue kwa utimilifu na wataalamu waendelea kuhamasisha jamii kulea watoto vizuri, akitaja kinachowagharimu wazazi, ni kukosa muda wa kuwalisha watoto, licha ya kuwapo chakula kwenye mlo huo.

"Watu wako 'bize' na mikopo na marejesho, tunataka tufanye kazi tujenge majumba tuwe na maendeleo, ila kumbe tusipowekeza kwa watoto, tutaambulia kuwa na watoto ambao hawako vizuri kwenye ubora wao," anasema Fisoo.

Katika Ripoti ya Utafiti wa TDHS-MIS 2022, Meneja Mradi wa Mtoto Kwanza, unaotekelezwa kutoka Shirika la COSITA mkoani Manyara, Agustino Balohho, anasema ripoti inatoa mwanga na dira kupunguza watoto waliokosa mwelekeo.

Balohho anataja maeneo ya kuboresha kwenye utafiti ni lishe kubaki changamoto, hata jamii inatakiwa kuhamasishwa namna ya ulaji na kuandaa chakula cha watoto.

"Wazazi wengi wanaangalia mwonekano wa mtoto siyo lishe ya mtoto na hawajui kuwa wanawapunja watoto kwa kuwanyonyesha chini ya miaka miwili, au kutokuwapa chakula kikamilifu," anasema Balohho.

Anataja wazazi wanaamini kunenepesha watoto na wanawekeza kwenye kutafuta fedha zaidi, kuliko kulea watoto.

Vilevile, kwenye ulinzi na usalama analalamika watoto wanaachwa kujilea na ukaribu nao unapungua, wazazi wakikimbizana na vikoba. Anaomba sheria kali kwa wabakaji na walawiti.

**MAONI YA WANANCHI**

Mwanakijiji wa Magara, Neema Daudi, anaasa ili wazazi wawalee vizuri watoto, wasiendekeza vya kisasa vinavyokiuka maadili.

Daudi anasema watoto wanakosa malezi bora ya wazazi wakitumia muda zaidi kwenye mitandao ya kijamii, akitoa mfano kinamama wanaotegemea wafanyakazi wa ndani kulea watoto wao.

Mkazi wa Mtaa wa Bagara Ziwani, Babati, Paul Sanka, anasema watoto kulelewa vizuri kunahitaji kutengewa muda wa kukaa nao, kuwahudumia na kuwasikiliza, akisisitiza muda kucheza, mlo kamili, vyote vinamaanisha afya.

Utafiti tajwa unaonyesha, vifo vinavyotokana na uzazi (MMR) Tanzania, viko 104 kwa kila vizazi 100,000. Miaka saba awali, uwiano huo ulikuwa vifo 149 kwa kila vizazi 100,000.

Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) ya 2021/22-2025/26, inasema serikali kupitia Sera ya Afya ya Mwaka 2007, imewekeza katika kuboresha uhai wa mtoto, kupitia utoaji huduma bure za afya kwa kinamama, wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

PJT-MMMAM inaeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuboresha Afya ya Uzazi, Mzazi, Mtoto na Vijana nchini mwaka 2016-2020, umeweka mazingira wezeshi kupunguza magonjwa, vifo vya kinamama, watoto wachanga, watoto na vijana kwa kutoa huduma bora.

**• Kwa mawasiliano na mwandishi, piga: 0628905182.**

AFYA

# Serikali inaandaa kampeni michezo ya rede, kuruka kamba viwanja vya shule

• Lengo kila mtu afikiwe ifikapo mwaka 2030

**Na Mary Geofrey**

WATU milioni 500 wanakadiriwa watakuwa wameugua magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kisukari, unene kupita kiasi na magonjwa ya moyo kutokana na kutofanya mazoezi ya mwili ifikapo mwaka 2030 duniani.

Ripoti iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika nchi 104, iliyotoka mwaka 2022, ina ufafanuzi huo.

Wizara ya Afya nchini, imeanza kuchukua hatua za kuhimiza umma kufanya mazoezi, ili kuepuka ongezeko la wagonjwa hao.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, anaiambia Nipashe kuwa orodha ya magonjwa hayo ni kisukari, saratani na shinikizo la juu la damu. Anasema chanzo ni tabia ya kutofanya mazoezi ya viungo na kuushughulisha mwili, ulaji usiyofaa, matumizi ya tumbaku na pombe kipita kiasi.

Dk. Ubuguyu anasema, hadi sasa ni miaka minne nchi iko katika kampeni kuhakikisha jamii inajikimu dhidi ya athari hizi tajwa za kiafya.

Anasema wamefanya upembuzi yakinifu, unaoonyesha kiwango cha watu kutoshughulisha mwili ni kikubwa na sehemu kubwa ya watu wanaoshughulisha ni wanaoshurutishwa na kazi, pia nyendo za maisha yao kila siku.

"Mfano mtu anatoka nyumbani anatembea hadi kituoni kufuata usafiri na akishuka anatembea hadi ofisini. Tayari ameushughulisha mwili, lakini kwa sababu ya kufuata usafiri," anasema.



Wanajamii wakifanya mazoezi katika viwanja vya Shule ya Msingi, Oysterbay, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

### HALI ILIVYO

Anasema walibaini asilimia sita ya Watanzania wanafanya mazoezi kwa ajili ya afya au kama burudani, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012.

Dk. Ubuguyu anasema kiwango hicho ni kidogo, kikionyesha Watanzania 96 kati ya 100 waliobaki hata kama wanafanya mazoezi, ilikuwa sio kusudio lao.

"Ukiwa huna fedha utabeba ndoo hadi chooni, ukiwa na fedha utaweka bomba hadi chooni, ukiwa una hela utalima, ukiwa nazo huwezi kulima kwa afya. Unalima kwa sababu huna namna lazima ufanye ili ule," anasema.

### KUHUSU KONGAMANO

Dk. Ubuguyu anasema, wanaandaa kongamano la kuanzisha kampeni kuhamasisha mazoezi, ikishirikisha Wizara za Afya, Michezo, Ardhi, Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Nchi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Pia kuna Baraza la Michezo la Taifa, vyama vya michezo, walimu na wataalam wa michezo kutoka Chuo Kikuu Shirikishi cha Afya Muhimbili (MUHAS), Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza, Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Mabalozi wa Usalama Barabarani na wanataaluma kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

> **Takwimu asilimia 9.1 sawa na kila watu 11 ana ugonjwa wa kisukari kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012.**

### MAENEO YA VIKWAZO

Dk. Ubuguyu anasema, mwaka 2019/20 walitathmini na kubaini hali ilivyo, wakipita maeneo 11 yanayo kuzorotesha mkakati wa ufanyaji mazoezi.

Hapo anasema walibaini hakuna maeneo ya kufanyia mazoezi ya kutembea na wanaotembea barabarani wapo hatarini kugongwa na magari, pia pikipiki.

Anasema, waliona barabarani jioni kunatumiwa na wajasiriamali, vyombo vya moto haviheshimu alama za barabarani kama zebra, maeneo mengi ya shule yamezungukwa na maduka, hata kukosesha watu fursa za kufanya mazoezi.

Dk. Ubuguyu anasema, wanajenga uhusiano mzuri na shule zenye miundombinu, upatumie kwa mazoezi, lakini wayatunze huku wakichangia kiasi kidogo shuleni.

Sasa anataka wapange mikakati kuanzisha michezo ikiwamo; rede, mpira wa miguu, kuruka kamba na mingine, vyote vikitarajiwa kusaidia afya ya umma.

### TAKWIMU ZILIVYO

Dk. Ubuguyu anasema watoto wadogo wanatakiwa kushughulisha mwili angalau kwa dakika 60, mara moja kwa siku na mara tano kwa wiki.

Anasema takwimu za watoto zinaonyesha asilimia 20 sawa na watoto wawili kati ya 10 tu ya wanaoshughulisha mwili inavyotakiwa na asilimia 20 hawafanyi kabisa mazoezi, akitaja ni kiwango hatarishi kwa afya yako.

Daktari huyo anataja sababu inachangiwa na watoto kukaa muda mrefu bila kushughulisha mwili, kucheza 'game' ya simu, kuangalia televisheni, kuangalia katuni na kusoma, akitaja ni kundi kuanzia miaka mitano hadi 18.

Anataja hatari yao ni maradhi ya kiharusi, hata shinikizo la juu la damu. Daktari Ubuguyu, anataja kundi la pili ni la watu wote na tatu wazee waliopo ofisini, kwa sababu hawapati nafasi ya mazoezi, hali kadhalika hospitali wamelala.

Pia, anagusa kundi la wenye ulemavu wanahitaji kufanya mazoezi, athari za magonjwa yasiyo ya kuambukiza zinaanza na miaka 40 na vichocheo vinaanza mapema siyo miaka hiyo na wengi wanashindwa kubaini.

### HALI YA MAGONJWA

Mtaalamu huyo wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, anasema huwa hayaanzi mara moja na kuzidiwa ni vichocheo vinatangulia miaka 10 hadi 20 nyuma.

Anasema, takwimu asilimia 9.1 sawa na kila watu 11 ana ugonjwa wa kisukari kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012.

Dk. Ubuguyu anasema, pia katika kila wanne, mmoja ana shinikizo la juu la damu na kila mwaka kuna watu 40,464 wanaugua saratani. Vilevile, kuna 26,000 wanafariki kila mwaka.

Anasema magonjwa yote yanaepukika, kwa sababu hayana gharama kuliko kutibu gharama za matibabu zinazoligharimu taifa.

Mtaalamu huyo anashauri kila siku, mtu anatakiwa kutembea dakika 30 kwa mwendo wa haraka.

### GHARAMA ZA MAGONJWA

Dk. Ubuguyu anasema, kuna watu wanaofariki, serikali inaingia gharama, moja kati ya tano wanaopoteza maisha wanafariki kabla ya miaka 60 hadi 70.

Anasema, theluthi ya pesa za wizara hiyo inatumika kuimarisha hospitali kwa ajili ya magonjwa hayo, akieleza zaidi ya shilingi bilioni 500 inaelekezwa kwenye sekta hiyo, sasa kukijengwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Ocean Road.

Anashauri kutembea kwa dakika 30 kila siku au dakika 10 kutembea mfululizo na kubadilisha ulaji wa chakula kula matunda na mboga na utaratibu wa kupima afya.

### WADAU WANASEMAJE

Mratibu wa Shirikisho la Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza, Happy Nchimbi, anafafanua shirikisho hilo lilianzishwa mwaka 2012, kwa lengo la kueneza uelewa kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Anasema, pia wanahamasisha na kuhimiza sera zinazopambana na kujikinga na magonjwa hayo na kuelimisha jamii, hata makundi mbalimbali ya walimu, wanafunzi, wafanyakazi kuwasaidia kisaikolojia. Happy anasema watoto wenye magonjwa ya kisukari kwa hatua ya kwanza wamewasaidia kupata dawa na kuwapata vitendea kazi vya kupimia sukari.

Anasema kwa sasa wameweza kushirikisha Baraza la Taifa la Michezo kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanna na Michezo kupitia mkakati walioounda wauhimize.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Addo Komba, anasema wameungana na Wizara ya Afya na wadau wengine kuandaa mpango kazi wa shughuli la mazoezi ya viungo ili kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Anasema katika kulisaidia Taifa kupambana na tatizo hilo, wanashirikiana wadau mbalimbali kuangalia namna ya kuanzisha na kuendeleza michezo shuleni, maeneo ya kazi na hospitali.

Mwakilishi kutoka MUHAS, Dk. Fredrick Mshiji, anasema lengo la mpango huo ni kuhakikisha kuna hali ya kuwezesha jamii kujihusisha na mazoezi ya mwili katika maisha ya kila siku.



# RC apiga 'stop' shughuli za ulinzi wa asili Mkalama

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI ya Mkoa wa Singida imepiga marufuku shughuli za ulinzi zinazotekelezwa na kikundi cha asili maarufu 'Nkili', katika Wilaya ya Mkalama.

Kikundi hicho kinadaiwa kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa mbalimbali wanaowakamata kinyume na jukumu lake.

Marufuku hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Peter Serukamba, wakati wa mkutano wa hadhara baina ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na wananchi wa Kijiji cha Yulansoni baada ya kupokea malalamiko dhidi ya kikundi hicho.

"Naomba niwaulize, Nkili ni nini, ajitokeze mtu hapa anieleze maana yake....je! bado mnataka kuendelea na hii Nkili?," alihoji Serukamba.

Baada ya kujitokeza kwa baadhi ya wananchi, akiwamo Thomas Omari, aliyetetea shughuli za kikundi ni kuweka hali ya ulinzi na usalama, huku wengine wakipinga, ndipo Serukamba akaagiza kupigwa kura za siri na kupiga marufuku hiyo.

Wakieleza malalamiko kwa kikundi hicho, wananchi walisema wamekuwa wakipewa adhabu mbalimbali ikiwamo kutozwa fedha, badala ya kuwafikisha watuhumiwa kwa mamlaka husika kama polisi na mahakamani.

Kutokana na hali hiyo, Serukamba aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za nchi ili kudumisha hali ya ulinzi, amani na usalama katika eneo lao.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Grace Selemani, aliishukuru serikali kwa usimamizi imara uliowezesha kufikia kwa makubaliano ya kumaliza utata wa mgogoro juu ya kikundi hicho cha jadi na serikali.



# Wanawake waitwa kupima afya bure

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Women Tapo (TWT), Lulu Yassin, amewaita wanawake kujitokeza kwa wingi kupima afya zao bure kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yanayotarajiwa kufanyika kesho katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Amesema upimaji huo utafanywa na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Aga Khan na Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA).

Akizungumza katika ofisi za Shirika la Mfuko wa Udhamini Wanawake Tanzania juzi, alisema katika maadhimisho hayo, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji.

Alisema hivi sasa baadhi ya wanawake wamekuwa wakikumbana na matatizo mbalimbali za kiafya ambapo katika siku hiyo, miongoni mwa magonjwa yatakayopimwa ni saratani ya shingo ya kizazi na matiti, lakini na upimaji wa afya ya akili.

"Niwasihi wanawake wenzangu tujitokeze kwa wingi siku hiyo, baadhi yetu tunaishi lakini hatujui tunaumwa na magonjwa gani, tujitahidi kuhamasishana tusherehekee tukiwa tunajua hali za afya zetu," alisema.

Lulu alibainisha kuwa, hadi sasa Taasisi ya TWT ina miaka mitano na inaendelea kuwawezesha na kuwainua wanawake wa masokoni katika hali ya kiuchumi na kijamii kwa kuwapa elimu, rasilimali na fursa za kiuchumi.

Alisema malengo waliyonayo ni kuwapa ujuzi wanawake katika masuala ya ujasiriamali, utetezi wa ufahamu wa sheria, haki, uongozi, rushwa ya ngono, afya, mazingira bora, usawa wa kijinsia na uboreshaji wa sera.

Aidha, alibainisha kuwa miongoni mwa matukio yatakayokuwa siku hiyo ni matembezi ya amani, maonyesho ya bidhaa na biashara kwa wanawake masokoni na wajasiriamali wengine, tuzo kwa wanawake mahiri wa masokoni, mafunzo ya ujasiriamali bila kusahau upimaji wa afya bure kwa wanawake.

Mratibu wa Masuala ya Jamii kutoka MEWATA, Dk. Asha Mahita, aliwasihi wanawake kujitokeza siku hiyo kwa kuwa, kulingana na takwimu zilizotoka mwaka huu, zilionyesha miongoni mwa magonjwa yanayoendelea kushika kasi kwa wanawake ni saratani ya shingo ya kizazi ikifuatia matiti.

"Tuweke utaratibu wa kupima afya zetu mara kwa mara, hii itasaidia kubaini tatizo ambalo linakusumbua. Baadhi yetu tumekuwa waoga, hii fursa tunapaswa tuichangamkie tujitokeze kwa wingi siku hiyo natarajia kuona wingi wetu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Marcus Mwemezi Foundation (MMF), Belinda Nendiwe, aliwashauri wanawake kuja kupima afya ya akili siku hiyo, kwani kutakuwa na madaktari bingwa wanaohusika na ugonjwa huo.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (wa pili kulia), akiwatambulisha kwa wananchi wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Yulansoni, Kata ya Kinyangiri Wilaya ya Mkalama jana, ili wasimamie ulinzi badala ya kazi hiyo kufanywa na jeshi la jadi maarufu kwa jina la Nkili, baada ya kulalamikiwa na wananchi kwa kutoa adhabu mbalimbali, ikiwamo fedha ambazo hata mapato yake hayaingii serikalini. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Ndugai akemea tabia vijiji kugawa ardhi kiholela

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Mstaafu, Job Ndugai, amekemea tabia ya serikali za vijiji kugawa ardhi ovyo iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya umma.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mlali kilichopo Wilaya ya Kongwa mkoani hapa, alisema: "Ardhi ya kijiji msitoe ile ni ya matumizi ya umma na hayo matumizi ya umma ni mengi yanazidi kuja huko mbele. Inaweza kuamriwa vyuo vijengwe au hospitali mtapeleka wapi hizo huduma? Watachukua wenzenu wenye nafasi."

Ndugai ambaye ni Mbunge wa Kongwa alisema serikali ya Kijiji haipaswi kugawa ardhi na kama taasisi yeyote inakwenda kwa ajili ya uwekezaji inunue ardhi kutoka kwa watu na siyo kugawa iliyochini ya Serikali ya Kijiji.

Aidha, aliwahimiza wananchi kutokana na kuendelea kuongezeka ni muhimu kutunza ardhi wasiuze hovyo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alipongeza Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kutoa sehemu ya Msitu wa Hado kurudi kwa wananchi.

"Eneo hili litakaporudi litumike kwa manufaa ya wananchi na siyo kuwagaiwa kwa watu wengine, tumeidai hii ardhi kwa muda mrefu tusiwape watu ambao hatufaidiki nao, ardhi haiongezeki ila watu wanaongezeka," alisema.

Alitaka TFS kuja na mikakati sahihi ya kuwainua wananchi wanaotegemea msitu huo kiuchumi kama ufugaji nyuki.

# Singida wazindua programu ya kumjali mtoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Singida imezindua Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM) lengo likiwa ni kumjali mtoto tangu hatua za awali.

Uzinduzi huo umefanyika juzi ukihusisha makundi mbalimbali wakiwamo walezi wa vituo vya malezi ya watoto, wataalamu na wawakilishi wa watoto kutoka shule tofauti za msingi.

Akizindua programu hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Dk. Adrianus Kalekezi, alitoa wito kwa wazazi kuhakikisha wanatoa malezi bora kwa watoto kuanzia ngazi ya awali.

Alisema mpango huo umelenga katika malezi na makuzi ya watoto katika maisha ya awali na wajawazito tangu siku ya kwanza za mtoto akiwa tumboni mpaka miaka nane na kwamba mpango huu umekuwa ukitekelezwa kuanzia ngazi za chini hadi kitaifa.

Alisema serikali imewekeza katika programu hiyo ili kuhakikisha watoto wanakuwa na misingi mizuri hasa katika afya na elimu na kutolea mfano wa shule za kisasa za awali na msingi zilizojengwa zikilenga kumwekea mazingira rafiki katika elimu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi wa Mkoa wa Singida, Edward Masero, alifafanua kuhusu sera na miongozo ambayo imelenga katika huduma ya MMMAM kama Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Mwongozo wa Kitaifa wa Lishe kwa Watoto Wadogo (2013), Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017-22) na miongozo mingine ambayo yote inalenga katika kumtengeneza mtoto tangu hatua ya awali.





# Gereza halina chumba maalum kuwahifadhi watoto, wajawazito

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

GEREZA la Ruanda lililopo jijini Mbeya, halina chumba maalum kwa ajili ya wanawake wenye watoto na wajawazito wanaotumikia adhabu mbalimbali, hali inayosababisha watoto wasiokuwa na hatia kuchanganywa na wahalifu.

Mkuu wa gereza hilo upande wa wanawake, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza, Grace Mbedule aliyasema hayo juzi alipokuwa anapokea misaada kutoka kwa makundi mbalimbali ya wanawake kwa ajili ya wafungwa.

Makundi yaliyopeleka misaada hiyo ni pamoja na Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi na Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya.

Grace alisema pamoja na kukosekana kwa chumba hicho maalum hata chumba kilichopo ni kidogo hali ambayo inasababisha msongamano wa wafungwa hao na hivyo kuhatarisha afya.

Alisema chumba kilichopo kinatosha wahalifu 15 pekee lakini kwa sasa wapo wahalifu zaidi ya 15 wakiwemo wajawazito na wenye watoto wadogo.

"Wale watoto hawana kosa lolote na hawajahukumiwa bali wanakuja kwa sababu wapo na mama zao, hata yule mtoto aliyeko tumboni hana kosa bali anakuja humu ndani kwa sababu mama yake amekosea," alisema Grace.

Hivyo, aliwaomba wadau wa maendeleo kusaidia ujenzi wa chumba hicho maalumu kwa ajili ya wafungwa wajawazito na wenye watoto wadogo ili kuyalinda makundi hayo.

Pia aliwashukuru wadau waliojitokeza kutoa misaada kwa ajili ya wafungwa hao na akisema watahakikisha misaada hiyo inawafikia wafungwa hao.

Mjumbe wa UWT Mkoa wa Mbeya, Paulina Mwalunenge alisema walitoa misaada hiyo kama sehemu ya kuwakumbuka wanawake wenzao ambao wanatumikia vifungo mbalimbali kwenye gereza hilo kuelekea Siku ya Wanawake Duniani itakayoadhimishwa Machi 8 mwaka huu.

Alisema walitoa misaada ya vitu mbalimbali ikiwemo sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kupakaa na nguo kwa ajili ya wanawake hao walioko gerezani hapo.

Alisema wataendelea kusaidia wanawake hao kwa nyakati tofauti ili kuhakikisha wanaishi vizuri wakiwa kwenye gereza hilo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi Mkoa wa Mbeya, Neema Kisanga alisema wataangalia namna ya kuwasaidia mitaji wanawake wanaomaliza vifungo magerezani mkoani humo ili waendeleze shughuli za kiuchumi.

Alisema hali hiyo itawasidia wanawake hao kuondokana na utegemezi na wasirejee tena kwenye makosa ambayo yatawafanya waingie tena kwenye matatizo.

Alisisitiza kuwa wataendelea pia kulisaidia kundi hilo kwa vitu mbalimbali vitakavyolisaidia kuendesha maisha yao wawapo gerezani.

## Madiwani walalamika uwiano utoaji fedha za bajeti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Mbeya wamewataka wataalamu wa bajeti kuzingatia uwiano katika utoaji wa fedha kwenye kata zao, ili kuhakikisha kata zote zinapata fedha sawa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Wakizungumza baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2024/2025 madiwani hao waliomba ofisi ya Mkurugenzi kupitia upya upangaji wa fedha zilizoelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ili kila kata ipate mgawo wake.

Diwani wa Kata ya Igoma, Endrew Mwaipopo alisema bajeti iliyowasilishwa haina mizani sawa kwani baadhi ya kata zimetengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zaidi ya mitatu ya maendeleo huku kata nyingine zikiwa hazina mradi hata mmoja.

Alisema baadhi ya kata kutotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo inaondoa imani kwa wananchi juu ya Serikali yao, hatua ambayo inawapa wakati mgumu viongozi hao kukutana na wananchi wao kwa kuwa kiu ya wananchi wao ni kuona maendeleo katika maeneo yao na si vinginevyo.

Diwani wa Kata ya Mjele, Tatizo Gunza, alisema kukosekana kwa mgawanyo sawa wa bajeti katika kata zao kunakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo wananchi wanaitarajia kutokana na ahadi ambazo zilitolewa na Serikali.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mwalingo Kisemba alisema watayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na madiwani hao lakini akaongeza kwa kuwataka kushirikiana na watendaji wengine kusimamia vema ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato katika halmashauri hiyo.

Kikao cha baraza la bajeti la madiwani limepitisha bajeti ya Sh. billion 71.6 kwa mwaka 2024/2025 ikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu na mapato ya ndani.




Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Peres Magiri (kushoto), Balozi wa Norway nchini, Tone Tinnes (wa pili kushoto), Mwenyekiti wa Taasisi ya Right Farm for The Future, Osmund Ueland (wa tatu kulia), Mkurugenzi Mkuu wa Yara, Winstone Odhiambo (wa pili kulia) na Meneja Biashara wa Kampuni ya Seed Kanda ya Kusini, Noel Shirima, wakizindua Kituo cha Maarifa cha Yara eneo la Ilula, mkoani Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema wakulima wadogo kituo cha mafunzo kikifunguliwa

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

NEEMA imewafikia wakulima wadogo mkoani Iringa baada ya kituo cha mafunzo ya kilimo kufunguliwa, ambacho kitawawezesha kupata elimu na ujuzi kupitia maonyesho ya vitendo ili kufikia kilimo endelevu, kuongeza mavuno.

Kituo hicho kikiwa na shamba darasa la mahindi lenye ukubwa wa hekta 350 lipo wilayani Ilula mkoani Iringa, kimezinduliwa na Kampuni ya Yara Tanzania ikishirikiana na Shirika la Farm For the Futer (FFF) na Seed Co. Ltd

Akifungua kituo hicho, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego alisema hatua hiyo ni chachu kubwa ya juhudi za serikali katika kuongeza upatikanaji wa elimu ya kilimo na msaada wa ugani hasa kwa wakulima wadogo.

Alisema kituo hicho kitawasaidia wakulima kukabiliana na tatizo la kufikia kiwango kikubwa cha uzalishaji wa mazao.

Dendego alitaja baadhi ya matatizo yanayowakabili wakulima wa Mkoa wa Iringa ni pamoja na ukosefu wa elimu ya kilimo na pembejeo kama vile mbolea, miundombinu mibovu, teknolojia nafuu.

Matatizo mengine ni wadudu na magonjwa, uhaba wa vyanzo vya maji, kukatika kwa soko, ukosefu wa mitaji na mazingira magumu ya hali ya hewa.

"Nimefurahishwa kuanzishwa kwa kituo hiki ambacho kitatatua changamoto nyingi zinazowakabili wakulima wetu, hususani katika utoaji wa huduma za ugani, ufumbuzi wa lishe ya mazao kwa njia ya utafiti na maonesho ya vitendo," alisema Dendego.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo alisema: "Kituo cha Mafunzo cha Yara kitakuwa mbia wa kuaminiwa na kuwapa wakulima wadogo elimu na ujuzi kupitia maonyesho ya vitendo, zana na usaidizi unaohitajika ili kufikia kilimo endelevu, kuongeza mavuno na kujenga maisha yenye mafanikio".

Alisema kituo cha Iringa ni miongoni mwa vituo saba vya mafunzo vya Yara, kwamba vingine vipo katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Kilimanjaro, Tabora, Manyara na Zanzibar.

Alisema vituo hivyo vinakuza ushirikiano wa kimkakati ili kukuza ukuaji zaidi ya kuuza mbolea, ikiwa ni pamoja na misaada ya kifedha, dawa za kuua wadudu waharibifu na teknolojia ya upimaji wa udongo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Seed Co. Limited, Clive Muganda alisema: "Tutaendelea kusaidia mipango inayoendesha matumizi ya utafiti na ujuzi wa pamoja juu ya afya ya udongo, uendelevu wa mazingira na kuimarisha minyororo ya thamani ya kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa mali shirikishi."

Mwanzilishi wa FFF, Osmund Ueland, alisema kuongezwa kwa kituo hicho kutaongeza kasi ya ndoto ya mradi huo kuwa kituo cha mfano kwa maendeleo ya jamii nchini Tanzania.



## Serikali yaanza kununua mwani kutoka kwa wakulima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu imesema Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) inayomilikuwa na serikali imeanza kununua mwani kutoka kwa wakulima visiwani Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa juzi na wizara hiyo, Shaaban Othman, wakati akizungumza na wakulima wa mwani katika Wilaya ya Kati Unguja ili kujua changamoto zinazowakabili.

Kikao hicho ni sehemu ya ahadi ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kuona zao hilo ambalo linalimwa na wanawake kwa asilimia 80 linakuwa mkombozi kwao.

Alisema kitendo cha serikali kuunda kampuni yake kwa kiasi kikubwa kimekuja kuleta ushawishi na ushindani kwa kampuni za watu binafsi kununua mwani kutoka kwa wakulima na siyo kampuni hizo kuacha kufanya kazi hiyo.

Alisema kilimo cha mwani ni cha kimkakati ambacho kimelenga kuwakomboa wanawake kiuchumi na ndiyo sababu zilisababisha serikali kuunda kampuni kwa ajili ya kununua mwani kwa wakulima.

Aidha, alizitaja juhudi nyingine ikiwemo serikali kujenga kiwanda cha kuchakata na kuongeza thamani ya zao la mwani ambacho kitakuwa na uwezo wa mahitaji ya zao hilo tani 30,000 kwa mwaka.

Alisema kwa sasa yamekuwepo mageuzi makubwa katika zao la mwani ambapo bei imeongezeka kwa mwani aina ya spinosoum ambapo kilo moja huuzwa kwa shilingi 500 hadi kufikia Sh.1,000 na bei ya mwani aina ya cottonia imepanda kutoka Sh.1,200 hadi Sh. 2,000.

**Kikao hicho ni sehemu ya ahadi ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kuona zao hilo ambalo linalimwa na wanawake kwa asilimia 80 linakuwa mkombozi kwao.**

# Jaffo: Changamoto 21 kati ya 25 za muungano zimetatuliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Suleiman Jaffo, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT), zimefanikiwa kutatua changamoto 21 za masuala ya muungano kati ya 25 zilizokuwa zikilalamikiwa.

Aliyasema hayo jana katika kikao kilichowakutanisha mawaziri wa SJMT na SMZ cha kujadili masuala ya muungano, kilichofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema viongozi wa pande zote mbili wamekaa pamoja kujadili changamoto nne za muungano zilizobaki na kuangalia namna ya kupatiwa ufumbuzi.

Waziri Jaffo alizitaja changamoto nne zilizobaki ni pamoja na suala la sukari, usajili wa vyombo vya moto, bodi ya pamoja na mgawanyo wa mapato iliyokua sarafu ya pamoja ya Afrika Mashariki.

Alisema mchakato wa kutatua changamoto hizo ulianza tangu mwaka 2000 ambapo hadi kufikia mwaka 2010 changamoto mbili zimetatuliwa, pia mwaka 2020 hoja tano za muungano zimetatuliwa.

Waziri Jaffo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutatua changamoto zilizobaki.

Aidha alisema viongozi wakuu wa nchi, mawaziri, makatibu wakuu na wataalamu mbalimbali wamefanya kazi kubwa ya kuchakata changamoto zilizokuwepo hadi kufikia mafanikio hayo.

Makamu wa Pili ya Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema, lengo la mkutano huo ni kuzungumzia changamoto zinazoikabili utendaji wa shughuli za serikali.

Alisema Rais Mstaafu, Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa uongozi wake aliwataka viongozi wa serikali zote mbili kukaa pamoja kujadili na kuyafanyia kazi matatizo yanayojitokeza, hivyo kikao hicho ni muendelezo wa vikao hivyo.

"Watu wengi duniani wanashangazwa na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kudumu kwa muda mrefu, suala ambalo linatokana na kukaa pamoja na kujadili changamoto zinazojitokeza kwa uwazi na kuzipatia ufumbuzi kwa pamoja" alisema Hamza.

Akitolea mfano wa mafanikio ya muungano wa Tanzania, alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zenye muungano wa zaidi ya nchi saba, unaendelea kudumu kutokana na uzoefu unaopatikana Tanzania na hivyo jumuiya hizo kuendeleza muungano wao.

Alisema changamoto nyingi zimeshatatuliwa, hivyo mkutano huo unatoa matumaini makubwa kupatikana kwa maslahi ya wananchi wa pande zote mbili pamoja na kuendelea kudumu muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao una takribani miaka 60 sasa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi wakizungumza na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, aliyefika Ikulu Migombani juzi, kwa ajili ya kutoa mkono wa pole, kufuatia kifo cha Rais mstaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyefariki wiki iliyopita na kuzikwa kijijini kwao, Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: IKULU**

# Ofisa ataja siri ya ufaulu wanafunzi katika mitihani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Elimu Sekondari wa Wilaya ya Kusini Unguja, Ali Fadhili Ali amesema afya bora na mazingira mazuri ya kujifunzia ndiyo msingi wa mwanafunzi kufaulu katika mitihani yao ya taifa na kuwa na viongozi wazuri wa baadae.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akifunga mafunzo ya usafi wa mwili, kinywa, vyoo, mazingira na jinsi ya kujitambua kwa wanafunzi wa Shule ya Mtule.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na mradi wa Food for the Hungary International (KFHI) chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Korea (KOICA).

Ofisa huyo alisema mwanafunzi ili afauru vizuri katika masomo yake muda wote anatakiwa kuwa mwenye nidhamu, afya bora na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Alisema wakati umefika kwa jamii hasa wazazi kuwandaa watoto wao wanapokwenda shule ili kuwa na afya bora na usafi wa mwili.

Alisema mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi siyo tu kwa sare zao za shule bali hata sehemu wanayowekwa wakati kujifunza ambayo yanatakiwa kuwa safi na salama.

Alisema katika kufikia mafanikio hayo ya kupata elimu katika mazingira mazuri ni lazima wanafunzi wenyewe wawe mstari wa mbele katika kutunza miili yao hasa wale wanafunzi wa sekondari.

Ali alisema kuna baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakipuuza suala la usafi wa mwili hasa kwa wanafunzi wa kiume jambo ambalo siyo sahihi kwa makuzi yao.

Alisema uwamuzi wa shirika la KFHI kuwapa mafunzo wanafunzi wa shule hiyo yanayohusu usafi wa mwili, mazingira na usafishaji wa kinywa na vyoo utawajengea uwezo wa kuzidi kujitambua nini wafanye katika kuitunza mili yao.

"Katika kufikia lengo la kutunza mazingira jamii inawajibu wa kushirikiana na wanafunzi katika kutunza mazingia ili kuondoa changamoto ikiwemo ya ukame" alisema Ali.

Naye mjumbe wa kamati ya shule hiyo, Tajo Hussen Juma, alisema iwapo wanafunzi watakuwa na utayari wa kuweka mazingira hali ya hewa nayo itakuwa nzuri wakati wote.

Alisema wanafunzi hao kwa kuwa walipewa elimu ya kujifunza juu ya jinsia hasa ya kujitambua na juu ya makuzi yao itawaepusha watoto na matumizi ya bangi na dawa za kulevya lakini pia kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji.

Baadhi ya wanafunzi waliopatiwa mafunzo hayo walisema yatawajengea umakini wa kusafisha mwili na kujitambua katika makuzi yao hasa kujiepusha na utumiaji wa dawa za kulevya na mimba za ututoni.

Ofisa Msaidizi wa KFHI, Judith Joseph Maduhu, alisema lengo la kutoa elimu kwa wanafunzi ni kuwawezesha wawe wasafi wakati wote ili kujifunza katika maeneo salama na kupata elimu bora.

Alisema tayari wameshakamilisha mafunzo kama hayo katika Shule ya Jendele, Fukuchani na Shule ya Jendele kwa upande wa Unguja kwa upande wa Pemba ni Shule ya Shumba Viamboni na Chwaka Tumbe.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**DEED POLL**
**The registration of the Document Act**
**(Cap. 117)**

By this Deed, I the undersigned, **EVELYNE M LYIMO** of P.O.BOX 178, Tanga Do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former names of **EVELYNE FREDRIC MAKELEMO,** in lieu thereof do assume form the date hereof the name of **EVELYNE M LYIMO.**

**AND**

That the names **EVELYNE M LYIMO** as it appears on my Member Card No. 106200178350 (NHIF) While **EVELYNE FREDRIC MAKELEMO,** as appears on my National Identity Card No. **19540719-21101-00001-15 (NIDA).**

**AND**

In pursuance of such change of my name, I hereby declare that I shall at all times herein after in all records, deeds and instruments, in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **EVELYNE M LYIMO** in liue of **EVELYNE FREDRIC MAKELEMO** so renounced as aforementioned.

**AND**

I hereby authorize and request all persons to designate, describe and address me by such assumed name of **EVELYNE M LYIMO.**

In witness whereof, I have hereunder signed my assumed names of **EVELYNE M LYIMO** in lieu of the relinquished names of **EVELYNE FREDRIC MAKELEMO** and **DELIVERED** by the said

EVELYNE M LYIMO
Who is known/identified to me by
........ day of February, 2024
Before me: J. MWAJOMBE
Signature ........
Qualification: RESIDENT
Address: P.O.Box 97 TANGA
RESIDENT MAGISTRATE TANGA

........
**EVELYNE M LYIMO**



**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS CAP 117**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

By this deed poll **I MARY MUZE KAJIRU** (new name) of P.O.BOX-MOSHI. Utterly renounced relinquish and abandon the use of my former name of **MARY ALOYCE MROSSO** (old name )in lieu of and substitution of my former name **MARY MUZE KAJIRU** (new name ).

Reason for changing the name is to abandon the name of **MARY ALOYCE MROS**O (name after marriage )which used to Retirement details to the name of **MARY MUZE KAJIRU**(name before marriage)which appears to the Citizen Identity Card with number **19510816257210000114.**

For the purpose of evidencing such determination. I hereby declare that I shall at all times here after in all records, deeds documents and other writing and in all actions suits and proceeding as well as in all Public and private dealings and transactions and on all occasions what so ever use and subscribe the said name **MARY ALOYCE MROSSO** (old name )so relinquished as afore said but by the name **MARY MUZE KAJIRU** (name name).

I hereby expressly authorized and require all and every person and whom so ever at all times after the date hereof to designate describe and address me by the adopted name of **MARY MUZE KAJIRU** (new name )accordingly .

In witness whereof I have abandoned my old name **MARY ALOYCE MROSSO** into **MARY MUZE KAJIRU** (new name).

In witness thereof I have set hand at MOSHI,
This 28 day of FEBRUARY 2024
Signed and delivered by the said.
**MARY MUZE KAJIRU** who is
Known to me personally / identified to me by
........
In my presence this 28 day of FEBRUARY 2024

........
**DEPONENT**

BEFORE ME:
Name GLORY JOSEPH TAIRO
Signature ........
Postal address 7549 MOSHI
Qualification ADVOCATE



# KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MODEST AKIDA WA STAR ATTORNEYS**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T196 DBT** CHASSIS NO : **RN81009723,** ENGINE **NO R20A1710884** AINA YA GARI NI HONDA STREAM,GREY KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/2914/2024.`**

# KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE FLORENCE MWALEMBA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 711AQE,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/4050/2024.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 4417 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: JENIFA KARAZE HERSON**

**By 1: SYLIVESTER B. JOHNBOSCO**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the T. KANIKI day of 27/03/2024.
Dated at......this 06 day of 013.2024

..............................
RESIDENT MAGISTRATE ..............
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 3197 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: BEATUS JOSEPH CHANGALA**

**By 1: STELLA JOSEPH MWANILWA**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 8 day of 3.2024
Dated at Morogoro this 05th day of MARCH.2024

..............
RESIDENT MAGISTRATE

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**(MASJALA NDOGO)**
**INAYOKETI MOROGORO**

**SHAURI LA ARDHI NA. 1167/2024**

**MIKALI ABDUEL MSUYA & ANOTHER......................MDAI**

**DHIDI YA**

**1. MAENDELEO BANK TANZANIA PLC..........................MDAIWA**
**2. BEST GROUP (T) LIMITED............................MDAIWA**
**3. ELIZABERTH DORIS MASI............................MDAIWA**
**4. ASSISTANT REGISTRAR OF TITLES......................MDAIWA**
**5. ATTORNEY GENERAL........................MDAIWA**

**KWA: BEST GROUP (T) LIMITED**

**POPOTE MULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba MDAI amefungua shauri la MADAI tajwa hapo juu katika mahakama hii.

Hivyo shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 21/03/2024 saa 03:00 asubuhi, ili kupangwa tarehe ya kusikilizwa. Hivyo basi unatakiwa kuwepo, au kuwasilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya rufaa hii.

Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri hili litapangwa tarehe ya kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na hatimaye uamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 02 mwaka 2024.

..............
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
MOROGORO


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Othman, Dorothy washinda ACT

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati Maalumu ya Uchaguzi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Joram Bashange, amemtangaza Dorothy Semu kuwa kiongozi mpya wa chama hicho baada ya kuibuka mshindi katika uchaguzi uliofanyika juzi kwenye ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Pia amemtangaza Masoud Othman Masoud kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Ismail Jussa Ladu na Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita.

Matokeo ya uchaguzi huo yalitangazwa jana viwanja vya Mabibo ulikofanyika mkutano wa hadhara ambao ulihudhuriwa na mamia ya wafuasi wa chama hicho. Askari wa Jeshi la Polisi walikuwa kila kona ya eneo kuhakikisha ulinzi unaimarika na matokeo yakatangazwa kwa amani.

Katika nafasi ya Kiongozi wa Chama, Semu alikuwa anachuana na Mbarara Maharagande ambaye baada ya uchaguzi, alikubali matokea akisema ameridhishwa na uchaguzi ulivyoendeshwa.

Jumla ya wajumbe waliopiga kura walikuwa 538 na Semu akaibuka mshindi kwa kupata 354 sawa na asilimia 65.7 huku Maharagande akipata kura 134 sawa na asilimia 34.3.

Othman alishinda nafasi ya Mwenyekiti kwa kupata 536 sawa na asilimia 96, huku Jussa akipata kura 480 sawa na asilimia 94.2 za makamu mwenyekiti Zanzibar na Mchinjita akivuna kura 517 sawa na asilimia 96.6 nafasi ya makamu mwenyekiti Bara.

Akizungumza baada ya kuibuka mshindi, semu aliishukuru familia ya chama hicho kwa kuonyesha ukomavu wa kidemokrasia kuanzia ndani na nje ya chama.

"Sasa tumemaliza uchaguzi tunarudi kazini. Tunapofanya uchaguzi lengo si kumpata mshindi bali atayekiongoza chama ndiyo maana kaulimbiu yetu inasema 'sote ni washindi'.

"Sasa tunaenda kuwasemea Watanzania kutokana na hali ngumu ya maisha na changamoto za kila siku zinazowaumiza. Tunaraudi nyumbani kuhakikisha tunajenga taifa la wote," alisema huku akishangiliwa.

Alisema ana kazi kubwa ya kuhakikisha wanachama wa ACT Wazalendo wanaandikishwa ili kushiriki uchaguzi mkuu na kwamba hatua iliyopo sasa ni kufanya maandalizi.

"Lengo letu ni kushika dola. Wakati ni sasa tusisubiri tena lakini ninaamini mbele yetu Kuna ushindi mkubwa," alisema.

Naye Othman alisema anawashukuru wanachama kwa kumwamini na kumshukuru Juma Duni Haji, aliyekuwa mwenyekiti wa chama ambaye alijiengua, hivyo kumpa nafasi ya kushinda kwa urahisi.

**Imeandaliwa na Halfani Chusi na Joyce Lameck**

# Biden, Trump waongoza kura ya mchujo Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MATOKEO ya kura ya mchujo katika zaidi ya majimbo 15 nchini Marekani, yanaendelea kutolewa na kuwaweka Rais Joe Biden na mpinzani wake Donald Trump katika nafasi ya kukutana tena katika uchaguzi mkuu baada ya kila mmoja kujizolea ushindi katika majimbo mengi.

Kura hiyo ya mchujo ndiyo itakayoamua wanasiasa hao kupeperusha bendera ya vyama vikuu viwili katika uchaguzi wa rais utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Rais Joe Biden kutoka Chama cha Democratic anawania muhula wa pili hakuwa na upinzani wenye nguvu na inatazamiwa kuteuliwa kuwa mgombea wa chama hicho.

Kwa upande wa Republican, rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump ndiye anatazamiwa kuwa mgombea na kuufanya uchaguzi huo kujirudia kwa wawili hao kupambana kama ilivyokuwa 2020.

Hadi jana asubuhi, Rais Biden tayari alikuwa ametangazwa mshindi kwenye majimbo kadhaa yaliyoshiriki kura hiyo ya maoni inayojulikana kama kinyang'anyiro cha Jumanne Kuu.

Biden alishinda majimbo ya Oklahoma, Virginia, Tennesee, North Carolina, Vermont na Iowa, Maine, Utah, Minnesota, Texas na Massachusetts.

Kwa upande wake Trump, amepata ushindi kwenye majimbo ya Oklahoma, Virginia, Tennesee, North Carolina na Maine.

Kutokana na matokeo hayo, amembwaga kwa mara nyingine mpinzani wake Nikki Haley ambaye ameshinda Massachusetts, Texas, Colorado na Alabama.

Tangu kuanza kwa kura za mchujo mnamo Januari, Trump ameshinda majimbo yote ikiwamo South Carolina ambalo ni jimbo la nyumbani kwa Nikki Haley.

Awali, Haley alipata ushindi wa kwanza kwa kunyakua Wilaya ya Washington DC.

Matokeo hayo yanayoendelea kutolewa huenda yataongeza shinikizo kwa Haley ambaye alikuwa balozi wa zamani wa Marekani kwenye Umoja wa Mataifa, kutangaza kujiondoa katika kinyang´anyiro na kumwachia Trump.

Kama Biden na Trump watapata ushindi wa jumla katika vyama vyao, wanasiasa hao wawili wenye umri mkubwa wataingia ulingoni na kupambana tena, licha ya wote wameshindwa kuibua msisimko miongoni mwa wapigakura wa Marekani.

Katika utafiti uliofanyika nchini humo, imeonyesha Wamarekani wengi wangependa kuwaona wagombea wengine katika uchaguzi wa mwaka huu.

Pamoja na ushindi wa kura alioupata Jumanne kuu, Trump atasubiri hadi Machi 12 kufahamu iwapo ametimiza idadi ya wajumbe wanaohitajika ili kuteuliwa kuwa mgombea wa Chama cha Republican. **DW**



Watu wakipita katika barabara iliyoharibiwa na mafuriko yalitokea nchini Malawi hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# Tanzania ya pili Afrika usalama mitandao

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni nchi ya pili barani Afrika kwa usalama wa mitandao, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama nchini (ICTC), amesema.

Dk. Nkundwe Mwasaga alibainisha hayo juzi alipozungumzia mafanikio, mipango na mikakati ya kukuza Tehama nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Mwasaga, kupaa kwa Tanzania katika usalama wa mitandao kunatokana na taarifa za Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kupitia Global Cybersecurity Index . Tanzania ni mjumbe wa Baraza Kuu la ITU.

Aliongeza kuwa mbali na kung'ara katika usalama wa mitandao, Tanzania imetajwa kuwa ya kwanza katika huduma ya ufikishaji huduma ya intaneti kwa kasi kwenye nyumba na majengo.

Hiyo ni kwa mujibu wa vipimo vya utayari wa nchi kuhusu mitandao (Global Network Readiness Index 2023) inayoandaliwa na taasisi za Portulans na Shule ya Biashara ya Said katika Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza.

Dk. Mwasaga alisema mafanikio hayo ni jitihada za ICTC katika kubuni, kukuza na kuendeleza kazi na programu bunifu za teknolojia.

"Tunajitahidi kutoa fursa kwa vijana kubuni kazi na programu mbalimbali za Tehama ili kuendeleza teknolojia hii na kuifanya Tanzania ya kidijitali," alisema Dk. Mwasaga.

Alisema katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa kidijitali, serikali kupitia ICTC inaendelea na mpango wa kujenga vituo vinane vya Tehama nchini.

Alisema lengo kubwa la kuanzishwa vituo hivyo ni kuhakikisha inasimamia nguzo tano ikiwamo kukuza vipaji bunifu katika Tehama na kupanua wigo kwa vijana kufanya ubunifu na kuendeleza.

Serikali kupitia ICTC inakusudia kujenga vituo vinane nchini vya ubunifu wa teknolojia vitakavyowezesha vijana na wananchi kwa ujumla kuvitumia kuboresha kazi zao za kibunifu.

Vituo hivyo vinatarajiwa kujengwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Tanga, Mwanza, Mbeya na Zanzibar.

"Huu ni mpango wa awali, lakini mkakati uliopo ni kujenga vituo katika mikoa yote na wilaya zote, ili wananchi wavitumie na kujifunza suala zima la teknolojia," alisema.

Kiongozi huyo alisema vituo hivyo vitajengwa katika maeneo ya shule ambavyo vitasaidia vijana nchini kuendelea kuibua vitu mbalimbali vinavyohusiana na teknolojia na kuendeleza, vitakuwa na uwezo wa kuingiza watu 200 kwa wakati mmoja.

Aliomba wadau mbalimbali kushirikiana katika kuanzisha vituo hivyo, lengo likiwa kukuza vipaji tofauti na kulinda kazi bunifu za kiteknolojia.

Dk. Mwasaga alisema watu wengi wamekuwa na hofu na akili bandia au akili mnemba (Artificial Intelligence – AI) kwamba inaweza kuwakosesha kazi, jambo ambalo alisema si kweli kwa kuwa AI inaleta tija na watu wakipewa ujuzi mpya kuhusu teknolojia hiyo itasaidia.

Alisema watajenga kituo cha AI kwa ajili ya kuendeleza wataalamu wa Tehama pamoja na kuwezesha mafunzo maalum ya wataalamu wa Tehama 500 ili kukuza na kuendeleza ujuzi wa Tehama nchini.

Inaelezwa kwamba ujenzi wa vituo hivyo ni sehemu ya vipaumbele 13 vya ICTC ambavyo vina lengo la kuleta mapinduzi ya teknolojia na ubunifu nchini.

# KLABU 14 LIGI KUU ZAPONGEZWA KUZIIMARISHA SIMBA, YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wadau mbalimbali wakitoa pongezi kwa Simba na Yanga kuingia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), imeibuka na kwenda mbali zaidi, ikizipongeza zingine 14 zilizobaki kwa kuzipa changamoto timu hizo hadi kufikia hapo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, amesema anazipongeza klabu zote za Ligi Kuu, ikiwamo 14 ukiondoa Simba na Yanga, ambazo zimefanya kazi ya kuzisukuma na kuzipa changamoto kweye ligi kitu kilichosababisha zifanye vema katika michuano ya kimataifa.

**Alisema changamoto iliyopo sasa ni kwa sababu msimu huu zimefanya vizuri, basi msimu ujao zinatakiwa zifanye zaidi ya hapo, huku jitihada zikifanyika kuona Tanzania ikiingiza angalau timu nne kwenye hatu za makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.**

"Tunazipongeza Simba na Yanga, lakini kwa umuhimu wa pekee tuzipongeza na timu nyingine 14 zizobaki kwani bila hizi kuzipa changamoto kwenye ligi huku wasingeweza kufanikiwa kufika hapo, hivyo ni imani yangu timu zote 16 za Ligi Kuu zimetekeleza wajibu wao.

"Hizi mbili zimetinga robo fainali, lakini zilizobaki zimeweza kuzisukuma Simba na Yanga kwa kuwapa mechi ngumu, na kwao ni kama mazoezi ya kukomazwa kwa ajili ya mechi za kimataifa," alisema Kasongo.

Alisema kilichobaki sasa ni kuona msimu ujao timu za Simba na Yanga zikisonga mbele zaidi, lakini pia Tanzania kuingiza angalau timu nne kwenye makundi.

"Hii ni kazi ambayo tumeianza miaka mitano iliyopita, na kila mwaka tumeonekana kuimarika hadi kufikia hapa. Msimu uliopita tuliona timu yetu moja, Simba ikicheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine Yanga ikacheza fainali ya Kombe la Shirikisho, na angalia tena msimu huu, zote mbili zimecheza ligi hii na zimetinga hatua ya robo fainali, kwa hiyo changamoto kwetu ni kubaki kwenye 'levo' hiyo kwenda juu zaidi, na tunataka angalau msimu ujao tuwe na timu nne hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa mbili na Kombe la Shirikisho tuwe na timu mbili," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

**ROBO HIYOOO...**



Mshambuliaji wa Bayern Munich, Harry Kane, akiifungia timu yake moja kati mabao mawili aliyofunga wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Lazio ya Italia juzi, Jumanne kwenye Uwanja wa Allianz Arena na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi wa jumla wa 3-1. Katika mchezo wa awali, Lazio ikiwa nyumbani ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Kundemba FC yajisikitikia Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kundemba FC imesema bado inahitaji kufanya vizuri zaidi katika michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar ili kujiondoa katika mstari hatari wa kushuka daraja.

Kundemba FC juzi ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya majirani zao, Mlandege FC katika mchezo wa raundi ya 20 wa ligi hiyo ambayo inaenda mapumziko kupisha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mchezo huo uliojulikana kama 'Majirani Dabi', ulichezwa katika Uwanja wa Mau A na kushuhudiwa na mashabiki wengi.

Kwa matokeo hayo, Kundemba FC imefikisha alama 20 ikiwa bado imesalia nafasi ya 13 wakati Mlandege FC wakifikisha alama 25 nao wakiendelea kusalia nafasi ya 10.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Kocha wa Kundemba FC, Ali vua Shein, alisema kutoka sare mchezo huo muhimu kwao haukuwa mpango wao hasa katika mechi hiyo ya mwisho kuelekea mapumziko.

Alisema tangu hapo awali walijua wananeda kucheza mchezo wa dabi ambao ni mgumu tangu timu hizo zianze kukutana katika Ligi Kuu Zanzibar, lakini matarajio yao ili kuwa ni kushindana ili kupata alama zitakazowatoa katika nafasi waliyopo.

Kocha huyo alisema timu yake ilicheza vizuri katika kipindi cha kwanza, lakini cha pili walizidiwa jambo lilosababisha wapinzani wao kusawazishiwa bao.

"Kasi ya mchezo ilivyoanza hasa kipindi cha pili, mashambulizi yote yalielekezwa katika lango letu jambo ambalo lilisababisha kurejeshewa bao, ingawa wachezaji wangu walijitahidi kuhakikisha tunapata la pili, lakini haikuwa bahati yetu," alisema.

Aidha, alisema kulingana na nafasi iliyopo timu yao katika msimamo wa ligi hiyo, wachezaji ambao watakuwapo Unguja katika kipindi ambacho ligi itasimama, itamlazimu kutoa mpangilio wa mazoezi kwa mchezaji mmoja mmoja.

Hata hivyo, alisema michezo kumi iliyobaki katika ligi hiyo watahakikisha wanafanya vizuri ili mpango wao wa kubaki Ligi Kuu utimie msimu huu.

# Kocha KMC aeleza kinachowatesa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Abdihamid Moalin (pichani chini), amekiri kuwapo kwa presha kubwa ndani ya timu yao kutokana na kutopata matokeo mazuri katika michezo tisa mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kati ya mechi tisa zilizopita ambazo KMC imecheza, imetoka sare michezo sita, suluhu na Singida Fountain Gate FC na Coastal Union, sare ya mabao 2-2 na Simba na Namungo FC na ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania na Geita Gold FC.

Mechi tatu walizopoteza walikubali kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Azam FC, wakaruhusu 3-0 dhidi ya Yanga na juzi walikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wenyeji wao, Ihefu FC mchezo uliopigwa katika Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Akizungumza na Nipashe jana, Moalin alisema wanatakiwa kupunguza presha waliyokuwa nayo kwa kutafuta matokeo mazuri katika mechi zilizopo mbele yao ikiwamo ijayo dhidi ya Tabora United.

Aidha, amekiri kuwapo kwa ugumu wa ligi katika mzunguko wa pili na kupambana kusahihisha makosa yao na kutafuta matokeo mazuri katika mechi zao zijazo ili kupunguza presha waliyokuwa nayo.

"Kuondoa presha iliyopo sasa ni kushinda mechi tulizokuwa nazo mbele yetu, juzi tumepoteza na Ihefu FC, tukiwa ugenini lakini tumerudi nyumbani kusahihisha makosa yetu kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Tabora United," alisema Moalini

Aliongeza kuwa katika msimamo wanashika nafasi ya tano ambayo si mbaya kwao, lakini kama wataendelea kushindwa kupata matokeo watazidi kujiweka katika wakati mgumu hali ambayo hawataki kuona ikitokea.

"Kushinda baadhi ya mechi zetu ndicho kinachoweza kututoa katika presha hiyo, hali ambayo wachezaji wanatambua umuhimu wa mechi zilizopo mbele yetu kupata matokeo mazuri na kuvuna pointi tatu kwa kila mchezo," alisema.



## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE AWINDWA UNITED

MANCHESTER United ilituma maskauti kumtazama mshambuliaji wa Bologna, Joshua Zirkzee, katika mchezo wao dhidi ya Atalanta Jumapili, ambaye pia anawaniwa na Arsenal na anaweza kugharimu kama euro milioni 80. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KIMMICH ATAKIWA CITY

MANCHESTER City inajiandaa kuipiku Liverpool katika kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich, 29, msimu huu. ***(Caught Offside)***

### LIVER YAVUTIWA NA NETO

LIVERPOOL inavutiwa sana na winga wa Wolves, Pedro Neto, 23, lakini wana wasiwasi kuhusu rekodi ya jeraha la mshambuliaji huyo wa Ureno. ***(Football Insider)***

### GUEHI KUUZWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inaandaa orodha ya wachezaji wanaolengwa wa nafasi ya mlinzi wa kati huku beki wa England, Marc Guehi, 23, akitarajiwa kuuzwa msimu huu wa majira ya joto kwa ada ya zaidi ya pauni milioni 50. ***(Telegraph)***

### AMORIM KUMRITHI XAVI

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, ndiye anayelengwa zaidi na Barcelona kurithi mikoba ya Xavi mwishoni mwa msimu huu, ingawa kocha huyo wa Ureno anaaminika pia kuwa na nia ya kujiunga na Liverpool. ***(Independent)***

### FRIMPONG AIVUTIA BAYERN

BAYERN Munich inavutiwa na mlinzi wa pembeni wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong, 23, ambaye ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka cha kati ya euro milioni 40 na euro milioni 45. ***(Sky Sports)***

### KELLY UHAMISHO WA BURE

KLABU ya Newcastle United ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly, 25, kwa uhamisho wa bure. ***(Mail)***

### BARCA KUMUUZA PEDRI

BARCELONA itasikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Hispania, Pedri, 21, msimu huu kwa sababu ya wasiwasi juu ya historia yake ya jeraha huku wakijaribu kusawazisha vitabu vyao vya mahesabu. ***(AS)***

### GREAVES AWANIWA EVERTON

EVERTON inamfuatilia mlinzi wa Hull City, Jacob Greaves, 23, huku kukiwa na nia ya kumnunua beki wa kati wa England, Jarrad Branthwaite, 21. ***(Mirror)***

### BARDGHJI LULU EPL

KLABU za Ligi Kuu England zinapigana vikumbo kumsaini Roony Bardghji, 18, wa Copenhagen mwenye thamani ya pauni milioni 20, huku Aston Villa, Newcastle United, Tottenham Hotspur na Manchester United zote zikimhitaji kiungo huyo wa kati wa Sweden. ***(HITC)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND ADOKEZA KUONDOKA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland amesema "anafuraha sana" ndani ya Manchester City, lakini mshambuliaji huyo ameacha mlango wazi kwa kuondoka hapo Uwanja wa Etihad siku zijazo.

**Haaland alisaini mkataba na Man City hadi mwaka 2027 baada ya kuwasili kutoka Borussia Dortmund kwa uhamisho wa pauni milioni 52 mnamo 2022.**

City wana nia ya kuafikiana mkataba mpya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, baada ya miezi 18 ya mafanikio ambayo imemfanya kufunga mabao 80 katika michezo 84 na kushinda Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Haaland alisisitiza kuwa ametulia katika klabu hiyo, lakini aliweka wazi kwamba kuna uwezekano wa kuondoka siku zijazo.

"Nina furaha sana," alisema Haaland akiwaambia wandishi wa habari juzi.

> ●●● Nikisema hivi sasa huenda kikawa kichwa kikubwa sana kesho huwezi jua italeta...

"Hasa na watu ambao nimezungukwa nao; kocha, wakurugenzi, bodi, ni kundi la watu wa ajabu na nina furaha sana, lazima niseme.

"Nikisema hivi sasa huenda kikawa kichwa kikubwa sana, kesho huwezi jua italeta nini, lakini nina furaha. Unaweza kuandika haya lakini pia unapaswa kuandika kila nilichosema hapo awali. Nina furaha. "

Haaland amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Real Madrid, ambao wanataka kumsajili Kylian Mbappe kutoka Paris Saint-Germain msimu huu wa majira joto.

Ripoti kutoka Hispania zimependekeza kwamba, licha ya mafanikio uwanjani, Haaland amechanganyikiwa na maisha ya Manchester, lakini raia huyo wa Norway alichukua nafasi hiyo kupunguza uvumi huo.

"Ninafurahia maisha. Ninafurahia maisha na watu wangu wa karibu na ninayafurahia. Sijui niseme nini kingine," aliongeza Haaland.

Haaland bado ana zaidi ya miaka mitatu kwenye mkataba wake, lakini City wangependa kuongeza mkataba angalau kwa msimu mwingine.

Atakuwa na umri wa miaka 27 wakati mkataba wake unamalizika na akasema anaangazia tu kipindi cha pili cha msimu akiwa na City badala ya mazungumzo ya kuongeza muda wake.

"Umakini wangu sasa ni uwanjani," alisema.

"Kuna michezo mingi. Siku mbili zilizopita ilikuwa Manchester dabi, sasa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumapili ni Liverpool, nadhani ninapaswa kuzingatia hilo. Sifikirii kuangazia kitu kingine chochote kwa sasa."



# TEN HAG HALI TETE UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wamefuatwa na wawakilishi wa makocha kadhaa wakiamini kwamba Erik ten Hag anaweza kuondolewa kwenye wadhifa wake kabla ya kuanza kwa msimu ujao, vyanzo vimeiambia ESPN.

Ten Hag yuko kwenye presha kutokana na kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Manchester City Jumapili na kuiacha timu yake ikiwa nafasi ya sita kwenye jedwali la Ligi Kuu England.

Mholanzi huyo ameambiwa kuwa kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ni muhimu kwa lengo la klabu hiyo kuwekeza kwenye kikosi msimu huu wa majira ya joto, huku pia akikidhi mahitaji ya faida na uendelevu, lakini matokeo ya Etihad yameifanya United kuporomoka kwa pointi 11 nyuma ya Aston Villa katika nafasi ya nne. Huku kukiwa kumebakiwa na michezo 11 ya kucheza.

Ten Hag amehusika kikamilifu katika kupanga majira ya joto -katika suala la kubainisha malengo ya uhamisho na kuandaa ziara ya kabla ya msimu mpya nchini Marekani - lakini chanzo kimoja kiliiambia ESPN kuwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, hajahakikishiwa rasmi na mmiliki mpya, Sir Jim Ratcliffe au timu yake kwamba atakuwa msimamizi msimu ujao.

Imehimiza mbinu kutoka kwa wasimamizi wasio na kazi na wengine ambao wako kwenye kazi kwa sasa ili kujua kama kutakuwa na nafasi.

United, kulingana na vyanzo, wamepokea habari juu ya kile makocha tofauti wamepanga kwa siku zijazo, na ni maslahi gani mengine katika kupata huduma zao, lakini hakujawa na majadiliano rasmi na wagombea wowote.

Liverpool, Bayern Munich na Barcelona zote zinatafuta makocha wapya kwa msimu ujao na, kulingana na vyanzo, kwa sasa wanafikiria chaguzi.

Timu ya Ratcliffe, inayoongozwa na Sir David Brailsford na Jean-Claude Blanc, bado inakamilisha maelezo ya muundo mpya Old Trafford, ambayo itaamua ni wasifu gani wa kocha wanataka kuchukua jukumu la kusimamia masuala ya kikosi cha kwanza.

# Pique ataka mashabiki Barca waambiwe ukweli

**BARCELONA,** Hispania

GWIJI wa Barcelona, Gerard Pique, ameionya klabu hiyo dhidi ya kuwahadaa mashabiki wao na kuihimiza klabu hiyo kuwa wazi kuhusu hali yao.

Barca ina takriban euro milioni 200 zaidi ya kikomo cha matumizi ya kila mwaka cha euro milioni 204 kilichowekwa na LaLiga, jambo ambalo linawazuia kusajili wachezaji wapya wanaoweza kusajiliwa au kuongeza mikataba mipya.

Uwanjani wameachwa kwa pointi nane nyuma ya vinara wa LaLiga Real Madrid na kutupwa nje ya Copa del Rey na Spanish Super Cup tangu mwanzoni mwa mwaka.

Wamebakia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku mechi yao ya mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora dhidi ya Napoli ikichezwa wiki ijayo, lakini Pique hajashawishika kuwa mambo yatakuwa mazuri kwa muda mfupi.

"Mashabiki wanataka uaminifu na uwazi," alisema beki huyo wa kati wa zamani wa Barca akikiambia kituo cha Twitch cha Ibai Llanos.

"Kama ukweli ni mgumu, sema. Kuwaambia kwamba, hatutashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa huna fedha za kushindana ni uongo.

"Sijui hali ya klabu kwa sasa -- kutokana na kile ninachoweza kukusanya haionekani kuwa nzuri - lakini kile wanachothamini jamii (wanachama) ni kuambiwa ukweli kwenye nyuso zao."

Moja kubwa chanya kwa Barca msimu huu ni kuibuka kwa vijana wenye vipaji kama Lamine Yamal, Pau Cubarsi na Fermin Lopez kutoka akademi yao.

Pique, ambaye alistaafu mwishoni mwa 2022, anaamini mashabiki wataelewa ikiwa rais Joan Laporta atasema klabu hiyo itazingatia wachezaji wa nyumbani huku ikirejea katika hali ya kifedha.

"Ukisema, 'tazama, hatuna hata senti ya kutumia, kwa hiyo miaka miwili au mitatu ijayo tutageukia La Masia,' watu watakubali," alisema.

"Ujumbe unapaswa kuwa kwamba tuna imani na akademi, kwamba kuna wachezaji wazuri na wenye vipaji vingi. Walete na ujaribu kushindana kwenye LaLiga."

# Kane aipeleka Bayern robo fainali Uefa

**MUNICH,** Ujerumani

MFUNGAJI bora wa Bayern Munich, Harry Kane alifunga bao katika kila kipindi na kuwawezesha Wajerumani hao kushinda 3-0 dhidi ya Lazio ya Italia Jumanne na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi wa jumla wa mabao 3-1.

Kane alifunga kwa kichwa dakika ya 38 kisha akafunga dakika ya 66 baada ya Thomas Muller kufunga kipindi cha kwanza kufanya kuwa mabao 2-0.

Ushindi huo unatoa ahueni ya papo hapo kwa kocha Thomas Tuchel na timu yake ambayo ilikuwa imeshinda mechi moja tu kati ya tano zilizopita katika michuano yote kabla ya Jumanne na kwa sasa wako pointi 10 nyuma kutoka kileleni mwa Bundesliga.

"Ni jioni nzuri sana kwetu. Ilikuwa mchezo mkubwa," alisema Kane, ambaye ameifungia Bayern mabao sita katika michuano hiyo na mengine 27 kwenye Bundesliga msimu huu.

"Tulikuwa chini kwa bao 1-0 katika mechi ya kwanza. Ni wazi kuwa ni wakati muhimu katika msimu wetu. Ilikuwa utendaji wa hali ya juu.

"Bila shaka tunajua tunapaswa kuimarika, lakini usiku kama huu unaweza kubadilisha msimu. Ninajivunia sana inabidi tuendelee na kasi hii."

Lazio walikuwa nyuma tangu mwanzo na walisubiri kuwapiga Wajerumani hao wakati wa mapumziko.

Bao la kichwa la Ciro Immobile lilikuwa nafasi yao bora zaidi, lakini lilitoka nje kidogo dakika moja kabla ya Kane kufunga bao lake la kwanza.



# Shime aitaka Tanzanite kuanza na 3 za Uganda

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasili salama nchini Ghana, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20 (U-20) Tanzanite, Bakari Shime, amesema lengo lake ni kupata ushindi katika mchezo wa kwanza wa mashindano ya All-Africa Games ya mwaka 2024, dhidi Uganda ili kujiweka kuongeza morali ya upambanaji kwa timu yake.

Tanzania inatarajia kushuka dimbani Jumamosi wiki hii kuvaana na Uganda ikiwa ni mechi ya kwanza ya kundi lao, mchezo utakaochezwa Uwanja wa Cape Coast Sports, nchini humo, katika mashindano hayo yanayoanza kutimua kuvumbi, Machi 8 hadi 23, mwaka huu.

Shime ameliambia Nipashe jana kuwa maandalizi walishafanya wakiwa Tanzania na kazi iliyopo sasa ni kukiweka sawa kikosi chake katika mambo madogo madogo ikiwamo kuwajenga kisaikolojia wachezaji kufikia mipango ya kusaka ushindi.

Alisema Uganda wana timu nzuri, lakini anaimani na vijana wake wameshika maelekezo yake, hivyo kwenda kuyatekeleza uwanjani kwa kukabiliana vema na wapinzani wao wakianza na Uganda.

"Kama nilivyosema awali kuwa hatutaenda na historia ya mpinzani wetu, bali tuweke mipango yetu imara na kutafuta ushindi katika mechi yetu ya kwanza dhidi ya Uganda kwa ajili ya kuanza vizuri michuano hii," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa licha ya kushiriki michuano mingi na kufanya vizuri anaimani All-Africa Games ni mashindano tofauti na wanahitaji kupata alama katika kile mechi kwenye kundi lao.

Tanzanite imepangwa Kundi A, ikiwa na timu ya Uganda , Ethiopia na mwenyeji Ghana. Mchezo wao wa Tanzania Baada ya mechi hiyo Tanzanite itarudi tena uwanjani Machi 12, kuvaana na wenyeji Ghana, katika na mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi itakuwa Machi 15, mwaka huu, dhidi ya Ethiopia itakayopigwa Uwanja wa Elmina.



# SERIKALI YAJA NA MWAROBAINI MIGOGORO SEKTA YA MICHEZO

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imesema haitaki kuona migogoro inaendelea kwenye vyama vya michezo kwani inarudisha nyuma maendeleo ya sekta hiyo nchini na katika kuhakikisha inapambana na hali hiyo sasa imekusudia kuja na mahakama ya usuluhishi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, alipokuwa anazungumza na viongozi wa vyama na mashirikisho ya michezo mbalimbali katika mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Alisema wanatarajia kujenga mahakama ya usuluhishi itakayokuwa na lengo moja la kusuluhisha migogoro hiyo ambayo haina tija katika maendeleo ya soka nchini.**

"Tunakwenda kujenga mahakama ya usuluhishi kwenye Ofisi za Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ambayo itakuwa inasuluhisha migogoro yenu kwani tunataka kuona michezo inafika mbali," alisema Ndumbaro.

Aidha, alisema ili kuhakikisha michezo inasonga mbele watarasimisha sekta ya michezo na kudai kwa wale watakaokiuka kanuni hizo watachukuliwa hatua kali.

"Kila kiongozi ahakikishe chama chake kinarasimishwa ili malengo ya sekta yetu yaonekane tukishrikiana kwa pamoja kwa kila kitu, inawezekana," alisema waziri huyo.

Aliongeza kuwa wameunda kamati mbili ambazo ni katiba mfano inayoongozwa na Mwenyekiti Leonard Tadeo, pamoja na ile ya mahusiano kati ya serikali na vyama vya michezo ambazo zitakutana ifikapo Juni mwaka huu mkoani Dodoma.

"Kamati ambazo tumeziunda tutakutana nazo mwezi wa sita baada ya kupokea mapendekezo yao tutayafanyia kazi," alisema.




Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, akizungumza na viongozi wa vyama na mashirikisho ya michezo katika mkutano uliofanyika Dar es Salaam jana kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta hiyo. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa wizara hiyo, Ali Mayay na kushoto ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo nchini (BMT), Neema Msitha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba yapigishwa kwata Morogoro*

INATOKA UKURASA 24

Sarr.

Haya hivyo, walikuwa Tanzania Prisons waliofanikiwa kuandika bao la pili dakika ya 61 kupitia kwa Mbangula baada ya makosa ya safu ya ulinzi ya Simba ndani ya eneo la hatari.

Kuingia kwa bao hilo ni kama kuliiamsha Simba walioanza kulishambulia lango la Tanzania Prisons, lakini wageni walikuwa imara kwenye kujilinda.

Dakika ya 89, Fabrice Ngoma, aliipatia Simba bao la kufutia machozi akiunganisha mpira wa kona uliowapita wachezaji wa Tanzania Prisons na kumkuta mfungaji.

Prisons walipata pigo dakika za mwishoni baada ya mwamuzi Nassoro Mwinchui kumwonyesha Haji Mussa Haji kadi ya pili ya njano iliyoambatana na nyekundu mchezo mbaya.

Kwa matokeo hayo, Tanzania Prisons wanafikisha pointi 27 kwenye nafasi ya sita ya msimamo wa Ligi Kuu huku Simba ikisalia nafasi ya tatu na pointi 36.

Mchezo unaofuata Simba watasafiri kwenda Tanga kukabiliana na Coastal Union na Prisons watasalia Morogoro kucheza na Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Manungu.

# Gamondi: Ligi Kuu silaha

INATOKA UKURASA 24

Gamondi aliwataka wachezaji wake wacheze mechi za Ligi Kuu kama ambavyo walikuwa wakicheza kwenye Ligi ya Mabingwa na wasiidharau timu yoyote kwani ushindi wa ligi ndiyo unaowapeleka kucheza mechi hizo kubwa.

"Kuna tabia ya baadhi ya wachezaji wakishapata ushindi kwenye mechi hizi kubwa morali yao inashuka na hawajitumi kwenye michezo ambayo wao wanaona ni midogo, hii si sawa, sehemu hii ndiyo timu inapata uwakilishi, tunahitaji pointi kila mchezo kupata nafasi ya kurudi tena mwakani, pia kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Gamondi.

Baada ya mechi hiyo, Yanga itakuwa nyumbani, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kucheza dhidi ya Ihefu, Machi 11, siku tatu baadaye, Machi 14, itashuka tena uwanjani hapo kucheza dhidi ya Geita Gold na siku zingine tatu baada ya hapo, Machi 17, itacheza kwenye uwanja huo dhidi ya Azam FC.

Hata hivyo, katika mechi hiyo, Yanga itakuwa mgeni kikanuni na baada ya hapo, itapata mapumziko ili kujiandaa na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajiwa kupigwa kati ya Machi 29 mpaka 31.

# Michezo

Alhamisi Machi 7, 2024

Nipashe




**Haaland adokeza kuondoka City** UKURASA 21



Mshambuliaji wa Simba, Freddy Michael, akimruka beki wa kati wa Tanzania Prisons, Nurdin Chona (chini), katika harakati za kutaka kufunga huku kipa wa timu hiyo, Yona Amos, akiwa imara na kuucheza mpira kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri, Morogoro jana na 'Mnyama' kuchezeshwa kwata ya mabao 2-1. **PICHA: SIMBA**

# Simba yapigishwa kwata Morogoro

**Na Faustine Feliciane,** Morogoro

## Ni kutoka kwa Tanzania Prisons baada ya kukubali kichapo katika...

MABAO mawili katika kila kipindi kutoka kwa Samson Mbangula, jana yalitosha kuwapigisha kwata Simba wakati Tanzania Prisons ikiondoka na pointi tatu kwa kuichapa 2-1 katika Uwanja wa Jamhuri mjini hapa.

Wakati Simba wakitoka kupata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, jana walishindwa kufurukuta mbele ya maafande hao wa Tanzania Prisons.

**Mbangula aliitanguliza Prisons dakika za majeruhi (45+3) za kipindi cha kwanza baada ya kukimbia na mpira na kuingia kwenye boksi na kupiga shuti lililomshinda golikipa Aishi Manula.**

Mpira ulianza kwa kasi kuanzia dakika ya kwanza ambapo timu zote zilifanya mashambulizi kwa zamu ambapo wageni Prisons walikuwa wa kwanza dakika ya tano, lakini shambulizi lao likaishia kwenye mikono ya Manula.

Dakika moja baadaye Simba walijibu mashambulizi ambapo shuti la Clatous Chama lilipaa juu ya lango la Tanzania Prisons.

Mpaka timu hizo zinaenda mapumziko Tanzania Prisons walikuwa mbele kwa bao hilo.

Kipindi cha pili kilianza kwa Simba kufanya mabadiliko kwa kuwatoa Kibu Denis, Freddy Michael na Mzamiru Yassin na nafasi zao kuchukuliwa na Ladack Chasambi, Saido Ntibazonkiza na Baubacar

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi: Ligi Kuu silaha tosha kwa robo fainali CAF

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mechi nne zilizopo mbele yake zinatosha kuwa mazoezi tosha ya kujiandaa na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Jumanne ijayo Yanga inatarajia kujua mpinzani wake wa hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati droo hiyo itakapochezeshwa nchini Misri majira ya saa tisa alasiri kwa saa za Afrika Mashariki.

Katika droo hiyo, Yanga inaweza kukutana na Petro de Luanda ya Angola, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ama Asec Mimosas ya Ivory Coast huku watani zao Simba wenyewe wanaweza kukutana na Al Ahly ya Misri, Mamelodi Sundowns ama Petro de Luanda.

Kocha huyo ambaye timu yake inajiandaa kucheza dhidi ya Namungo kesho, Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, amesema michezo minne iliyopo mbele yake itakuwa ni ya kuwaandaa wachezaji wake wawe fiti kwenye mechi hiyo ya kimataifa.

"Tumerejea kwenye mechi za ligi ambazo tutazitumia kutafuta ushindi, lakini hizi hizi tutatumia kujiandaa na mechi za robo fainali, zitatufanya tuwe imara, na Machi 12 droo itakapopangwa tutaongeza kitu kingine, nacho ni kujua mpinzani gani tutacheza naye na kuanza mazoezi maalum kwa ajili ya kumkabili kutokana na mbinu zao tutakazozisoma," alisema Gamondi.

Alikiri kuwa michezo ya kimataifa huwa ni migumu na yenye mbinu zaidi, lakini atafanya kila njia kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa kwa wachezaji wake.

"Mechi za makundi zilikuwa ngumu na ushindani mkubwa, lakini vijana wamepambana kwa kila hatua na kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali kwa kuvuka malengo yetu," alisema.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >